# BARAZA LA WAWAKILISHI
# ZANZIBAR

**Simu ya Upepo: Baraza**
**Nambari ya Simu:2230234/5**
**Tele Fax. Nam. (024)2230215**

**SANDUKU LA BARUA 902,**
**ZANZIBAR**

## RIPOTI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE

## NA USTAWI WA JAMII

**KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012**

**1.0 UTANGULIZI**

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 104(d) cha kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2011.Majukumu ya Kamati yameelezwa katika kanuni ya 110 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kama yafuatayo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kushughulikia Miswaada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ina jukumu la kufuatilia utekelezaji katika Wizara tatu nazo ni kama ifuatavyo:-

1) Wizara ya Afya

2) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

3) Wizara yaUstawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watoto

**1.1 WAJUMBE WA KAMATI**

Kamati inawajumbe wanane na makatibu wawili kama wafuatavyo-:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe.Amina Iddi Mabrouk. | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hija Hassan Hija. | Makamo Mwenyeki |
| 3. | Mhe.Asha Abdu Haji. | Mjumbe. |
| 4. | Mhe. Ashura Sharif Ali. | Mjumbe. |
| 5. | Mhe. Mwanaid Kassim Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe .Jaku Hashim Ayoub. | Mjumbe |

7. Mhe .Nassor Salim Ali. Mjumbe

8. Mhe. Saleh Nassor Juma Mjumbe

9. Ndg. Asha Said Mohamed. Katibu

10. Ndg. Talib Enzi Talib. Katibu

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 imefanya kazi zake kwa muda wa wiki sita.Kwa upande wa Unguja ilifanya kazi wiki mbili, kuanzia tarehe 19/09/2011 hadi tarehe 30/09/2011.Kwa upande wa Pemba ilifanya kazi wiki mbili kuanzia tarehe 12/12/2011 hadi 23/12/2011. Aidha Kamati ilifanya kazi wiki mbili kwa upande wa Unguja kuanzia tarehe 20/02/2012 hadi 02/03/2012. Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipata fursa maalum kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ya kufanya ziara ya ziada baada ya muda maalum wa kazi za kamati mjini Dar Es Salam kutembelea taasisi zilizo katika sekta ya Elimu katika Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 5 na 6 March ,2012 ili kujifunza na kuelewa maendeleo pamoja na changamoto zinazozikabili taasisi hizo katika sekta ya elimu nchini.Taasisi hizo ni Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi(NACTE),Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania(TCU) na Bodi ya Mikopo Tanzania.

## 2.0 UFUATILIAJI WA KAZI KATIKA WIZARA

## 2.1 WIZARA YA AFYA

## 2.2 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA MWAKA ULIOTANGULIA

Kamati kupitia Ripoti yake ya mwaka 2010/2011 ilitoa maagizo mbali mbali ambayo yalihitaji kutekelezwa na Wizara ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

- **Wizara ihakikishe kuwa Hospitali ya Wete inakuwa na chumba cha kuhifadhia maiti.**

Wizara imeandaa mkakati wa kutanua majengo ya Hospitali ya Wete kwa ufadhili wa Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo vitokanavyo na Uzazi(SMMRP) kupitia ADB, katika mkakati huo imejumuisha na suala la ujengwaji wa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali hiyo,hivyo inategemea kuwa na chumba cha kuhifadhia maiti itakapofanyiwa utanuzi wa majengo.

- **Serikali itafute ufumbuzi wa haraka wa tatizo la kukosekana kwa madaktari wa kutosha katika Hospitali ya Wete, ChakeChake, Mkoani na vituo vya Afya.**

Katika kuhakikisha madaktari wa kutosha wanapatikana katika Hospitali hizo na vituo vya Afya, Wizara kupitia Idara ya Tiba imefanya mazungumzo na kikundi cha Madaktari wa kujitolea (VSO) na makubaliano yaliyofikiwa ni kupatiwa madaktari bingwa wa fani mbali mbali kama Daktari bingwa wa ganzi, Daktari bingwa wa kinamama kwa Hospitali ya Vitongoji na Daktari bingwa wa upasuaji kwa Hospitali ya Wete. Pia Wizara imefanya mazungumzo na Ubalozi wa Cuba na kuomba watupatie madaktari na Ubalozi huo umeahidi kuipatia Wizara madaktari bingwa wa kada mbalimbali.

Vilevile katika kuhakikisha tatizo hili linapatiwa ufumbuzi, maombi ya kuwaomba wataalamu wa kada mbalimbali yamepelekwa Utumishi wa Umma katika Nominal Roll na maombi yamekubaliwa hivyo kinachosubiriwa ni kupata idhini ya nafasi zitakazotolewa ili kuanza hatua za uajiri.

- **Fedha zinazopatikana kupitia Mradi wa Ukimwi zionyeshwe katika bajeti ya Serikali ili Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali aweze kuzikagua.**

Fedha zinazopatikana katika Mradi wa Ukimwi zinaripotiwa katika bajeti ya Serikali kupitia MTEF, ambao unaonesha fedha za Serikali na za Wahisani. Hivi karibuni Wakaguzi wa nje (External Auditors) na wa Serikali walipata nafasi ya kutembelea na kuhoji kuhusiana na fedha za Mradi ikiwemo Mradi wa kudhibiti Ukimwi,na walipatiwa ufafanuzi wa hoja walizotoa.

Pia mradi unaendelea kuwasilisha ripoti za fedha za wahisani kwenye Idara ya Fedha za Nje Ofisi ya Rais Fedha,

Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambapo kila mwezi hufanyika vikao vya Aid Coordination kwa lengo la kuangalia bajeti na matumizi ya fedha za wahisani kwa kila mwezi.

- **Kamati imeagiza Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya utafiti wa kina na upembuzi yakinifu juu ya maji taka yanayoingia baharini na kuathiri viumbe hai vya bahari pamoja na watumiaji.**

Agizo hili bado halijatekelezwa.

- **Wizara imeagiza kufuatilia nyumba na vituo vya Afya vilivyojengwa na Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo vitokanavyo na Uzazi (SMMRP) kupitia ADB vinavyoanza kufanya nyufa juu na katika sakafu ili kuepuka uharibifu wa mapema.**

Tatizo la kufanya nyufa katika vituo na nyumba za madaktari tayari limeshajulikana na uongozi wa Mradi, hivyo ziara za kukagua vituo na nyumba za madaktari zote za Unguja na Pemba zimepangwa kufanyika mwezi wa Mei 2012, kwa nia ya kuangalia ubovu na mapungufu yaliyojitokeza ikiwemo nyufa katika sakafu na kuripotiwa kwa Mkandarasi kwa matengenezo, kwani mradi wa ujenzi wa vituo na nyumba za Madaktari umo katika dhamana ya Mkandarasi na anamaliza muda wake ifikapo mwezi wa Juni 2012.

Kwa hivyo, Mkandarasi anatakiwa akamilishe mapungufu yote yaliyojitokeza katika vituo na nyumba za madaktari na kukabidhi majengo kwa Mradi,na Mradi ukiridhika na ujenzi huo ndio atapatiwa cheti cha kukamilisha (certificate of completion).

- **Wizara iwe makini na iharakishe kazi za usajili waganga wa jadi wa tiba mbadala na maduka ili kuepuka kutoa huduma kiholela.**

Wizara kwa upande wa Pemba imechukua hatua za kukutana na viongozi wa Shehia kama vile masheha, madiwani na watu mashuhuri na kuwafanyia mikutano, kutoa miongozo katika vyombo vya habari ili kuifahamisha jamii umuhimu wa tiba asilia.Kazi ya kuwasajili waganga wa jadi wa tiba mbadala na maduka ya dawa unaendelea ambapo wahusika hutakiwa kuwa na vibali vya uthibitisho kutoka kwa sheha wa shehia wanayoishi.Waganga wa tiba asilia waliosajiliwa na kupata shahada ni 82,waliopata vibali kwa ajili ya kufanya tiba asilia ni 27 na waganga waliopata mafunzo ni 85.

## 2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YAMAENDELEO

### 2.3.1 MRADI WA AFYA YA AKILI

**Fedha za Mradi shilingi 70,130,000/=**

Katika kipindi cha Julai-Disemba, 2012 mchango wa fedha za nje za Mradi wa Afya ya Akili ni shilingi 11,669,000 /= ambapo fedha za ndani (SMZ) ni shilingi 11,669,000/=

**Utekelezaji wa malengo:**

- **Uendelezaji wa ukarabati wa majengo ya Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu.**

  Majengo yaliyofanyiwa matengenezo ni wodi nambari 1 na 2 ya wanaume, uimarishaji wa bustani na majengo mapya (jengo la utawala na huduma za matibabu ya nje na jiko).

- **Kukinga matatizo ya Afya ya Akili na ya Mfumo wa Fahamu**

  Upatikanaji wa dawa za matibabu ndani na nje unaridhisha isipokuwa kuna baadhi ya dawa imekuwa sugu kupatikana kama vile vidonge vya Haloperidol na Thioridazine.

- **Kukuza Afya ya watu wenye Matatizo ya Akili, Kimwili na Kijamii**

  Mafunzo kwa watoa huduma ya afya ya akili yamefanyika kwa upande wa Pemba ambapo jumla ya wafanyakazi 22 walishiriki kwa muda wa siku 5.

- **Kutoa huduma za afya ya akili katika hatua zote zikiwa ni pamoja na zile za ndani ya hospitali na vijijini kwa kuzingatia upatikanaji wa matibabu pamoja na huduma za marekebisho hasa kwa kinamama na watoto, pamoja na vifo kwa watu wenye matatizo ya afya ya akili**

  Huduma za ndani na nje zinaendelea, ikiwa ni pamoja na zile za kulaza wagonjwa. Kwa upande wa huduma

za vijijini, Mradi umejishughulisha na kutoa huduma karibu na wagonjwa kwa wilaya zote.Takwimu zinaonesha kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Disemba 2011 jumla ya ziara 45 zilifanyika na idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma ni 799(wanawake 421 na wanaume 378).

- **Kuanza utekelezaji wa ujenzi wa wagonjwa wa akili Wete , Pemba**

Katika hatua iliyofikia Mradi unaendelea vizuri.

**Changamoto:**

- o Fedha za mchango wa SMZ katika mradi ni ndogo ukilinganisha na makisio yaliyopangwa.
- o Hakuna uhakika wa upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa wa akili

### 2.3.2 MRADI WA MABADILIKO YA SEKTA YA AFYA, ZANZIBAR (HSRS)

**Fedha za Mradi ni shilingi 92,840,000/=**

Katika kipindi cha Julai-Disemba, 2011 mchango wa fedha za nje kupitia DANIDA za Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya Zanzibar ni shilingi 116,998,992 /= ambapo fedha za ndani (SMZ) ni shilingi 36,210,000/=

**Utekelezaji wa malengo:**

- **Utayarishaji wa zana za utekelezaji wa mkakati wa Afya ya Jamii**

  Kamati inayosimamia utekelezaji wa Mkakati wa Afya ya Jamii kwa kushirikiana na kitengo cha Elimu ya Afya, wameandaa Muongozo wa mawasiliano kwa ajili ya kamati za afya na viongozi wa shehia ili waweze kutekeleza Mpango wa Mkakati wa Afya ya Jamii kwa umahiri.

  Kazi ya kuchapisha mkakati huo na kuwasilisha katika ngazi ya wilaya na shehia na kuanza kutumika rasmi imepangwa kufanyika katika mwezi wa Machi, 2012

- **Kuandaa mpango wa muda mrefu wa jinsi ya kugharamia Sekta ya Afya (Long Term Financial Option)**

  Katika utekelezaji wa lengo hili ,hatua iliyofikiwa ni kuundwa kwa Kamati inayohusisha Sekta ya Afya ,Utumishi na Utawala Bora ,Shirika la Bima la Zanzibar,Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

  Kamati hiyo inakusudia kutekeleza yafuatayo kabla ya kumalizika mwaka wa fedha wa 2011/2012 chini ya ufadhili wa Shirika la Afya Duniani:

  - o Kufanya utafiti juu ya utayarishaji wa muamko kwa wafanyakazi wa serikali na jamii kwa jumla
  - o Kutafuta mshauri muelekezi ili kufanya “Design” na “Cost Insurance Scheme.”

- **Kuandaa Muongozo wa Rufaa ili uweze kutumika Hospitalini**

Wizara imemteua mtaalamu mmoja kwenda katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Tanzania Bara, kuonana na Katibu Mkuu na kuomba kusaidiwa suala hilo.Hii ni kutokana na kukosekana kwa Mshauri Mwelekezi kutoka Zanzibar.

**Changamoto**

- Kutokana na uzito wa utendaji wa kazi,pamoja na umuhimu wa Ofisi ya Sekretarieti ya Mabadiliko ya Sekta ya Afya katika kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wizara,unahitajika msaada mkubwa kutoka katika taasisi za kimataifa jambo ambalo hugharimu fedha nyingi na kupelekea kushindwa kutekeleza baadhi ya kazi walizojipangia.

### 2.3.3 MRADI WA CHUO CHA MADAKTARI CHA ZANZIBAR

**Fedha za Mradi zilizopangwa SMZ Tsh 240,800,000/=**

**Fedha za Mradi zilizopatikana Julai - Disemba SMZ Tsh 49, 477,050**

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MRADI:**

**Kukifanya Chuo kutambulikana Elimu ya Juu Tanzania**

Katika kutekeleza lengo hili maombi yamewasilishwa katika Taasisi ya Vyuo vya Elimu ya Juu.Chuo kimetumia kiasi cha shilingi 2,230,000 kwa ajili ya kupitisha Mpango mkakati wa Chuo.Hatua iliyofikiwa sasa ni Chuo kimepewa maeneo ya kuyafanyia kazi na kuwasilisha baadhi ya nyaraka kama vile taarifa binafsi za walimu (CV), Mpango mkakati na Mtaala wa Chuo.

**Kushirikisha madaktari wazalendo katika utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi**

Kwa hatua ya mwanzo ya utekelezaji wamepatikana madaktari 6 watakaoshirikiana na madaktari wa Cuba katika kuimarisha huduma za taaluma katika Chuo.

**Kununua vitendea kazi bora kwa maendeleo ya Chuo na wanachuo kwa ujumla.**

Chuo kwa kushirikiana na "Italian Cooperation" kimefanikiwa kununua vitendea kazi mbali mbali kama vile kompyuta 15, mashine za kutolea fotokopi 2, Printer 2, Projector 3 pamoja na vitabu.

**Ufuatiliaji wa upatikanaji wa miundo mbinu bora ya utekelezaji wa shughuli za Chuo**.

Chuo kimeweza kufanya ukarabati wa chumba cha kompyuta, kununua samani kwa ajili ya matumizi ya chumba hicho, pamoja na ukarabati wa Mfumo wa mtandao (internet) ambapo jumla ya shilingi 3,497,500/= zilitumika.

**Changamoto:**

- Eneo la Chuo ni dogo sana kiasi ambacho ni vigumu kuweza kuchukua wanafunzi wengine wapya (new intake) kutokana na upungufu wa majengo. Kwa upande wa Unguja kwa mfano, kuna madarasa 2 tu ambayo kwa sasa yanatumika kwa wanafunzi waliopo.
- Ukosefu wa usafiri kwa ajili ya wanafunzi
- Ukosefu wa wafadhili katika Mradi, hali ambayo hupelekea Chuo kutegemea fedha za serikali tu ambazo kwa kweli hazitoshelezi.

**2.3.4 MRADI WA KUPUNGUZA VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI**

**Fedha za Mradi zilizotengwa kwa mwaka 2011/2012**

**SMZ Tsh 100, 40,000/=, ADB 227,705,000/=**

Fedha zilizotolewa Julai-Disemba kutoka SMZ Tsh.30, 088,000.

**Utekelezaji wa Malengo**

**Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 10 wa Chuo cha Taaluma za sayansi za Afya Mbweni**

Mwalimu mmoja kutoka katika Chuo hicho ameshiriki mafunzo ya miezi 3 Tanzania Bara juu ya Mipango na Tathmini.

**Kugharamia mafunzo ya kipindi cha mwaka mmoja kwa walimu 3 na wafanyakazi wengine kutoka Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Mbweni**

Walimu 2 wamepelekwa Chuo cha CEDHA–Arusha kwa masomo ya mwaka 1ya Diploma ya Ualimu**.**

**Kusimamia ujenzi na kulipatia vifaa na samani jengo la huduma za Afya ya Akili Pemba.**

Ujenzi unaendelea vizuri.Mchakato wa ununuzi wa vifaa na samani umeanza kwa kuorodhesha mahitaji yanayohitajika**.**

**Changamoto**

- Tatizo la kupata nafasi za masomo katika Vyuo vya Tanzania Bara kulingana na idadi ya wanafunzi iliyopangwa katika vyuo husika.
- Kukawia kupata "no objection'' kutoka makao makuu ya ADB baada ya kutayarisha kazi zinazotaka kufanywa (BOQ) na mtaalamu wa majenzi.

**3.0 UTEKELEZAJI WA MATUMIZI YA FEDHA**

**Fedha za Kawaida (Reccurent Account)**

Wizara ya Afya ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh 10,727,000,000.00 kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Tsh.2, 100,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Tsh. 8,627,000,000.00 mishahara na maposho.

Mpaka kufikia Disemba 2011 jumla ya Tsh.6,122,965,311 ziliingizwa.Tsh.5,474,189,311 kwa ajili ya mishahara na maposho,sawa na asilimia 63 ya bajeti yake na Tsh.648,776,000.00 kwa kazi za kawaida ,sawa na asilimia 31 ya bajeti yake.

**Fedha za Maendeleo (Development Account)**

Kwa upande wa fedha za Maendeleo ,Wizara ya Afya iliidhinishiwa jumla ya Tsh.2,500,000,000.00.Hadi kufikia Disemba 2011 jumla ya Tsh.784,000,000.00 ziliingizwa ,sawa na asilimia 31 ya bajeti yake.

**Mapato**

Kwa upande wa ukusanyaji wa Mapato ,Wizara ya Afya imekadiriwa kukusanya jumla ya Tsh.537,000,000.00.Hadi kufikia Disemba 2011,jumla ya Tsh.110,966,484 zimekusanywa ,sawa na asilimia 21 ya bajeti yake ,na kuingizwa katika mfuko mkuu wa Serikali.

**3.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA**

Wizara ya Afya ina Idara 8, taasisi na bodi mbali mbali. Idara ya Sera, Mipango na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Kinga na Elimu ya Afya, Idara ya Tiba, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mkemia Mkuu wa Serikali, Mfamasia Mkuu wa Serikali, Idara ya Bohari kuu ya Madawa na Afisi ya Mdhamini Mkuu wa Wizara ya Afya Pemba. Wizara pia ina Taasisi mbali mbali kama vile Maabara ya Afya ya Jamii ilioko Pemba, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Bodi ya Wauguzi na Bodi ya Huduma za Hospitali Binafsi.

Idara husimamia utekelezaji wa Mpango wa Wizara kwa kuzingatia maeneo yaliyoainishwa kwenye Sera ya Afya 2011, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020, pamoja na Mpango wa Mkakati (Strategic Plan II 2006/7- 2011).

**Utekelezaji halisi:**

**a). Kuweka mfumo utakaoainisha mgawanyo wa wafanyakazi wa afya ambao utazingatia taaluma walizonazo na kwa kuzingatia mahitaji ya sehemu**.
Wizara imeunda kamati itakayoshughulikia kazi hii na tayari hadudi rejea zimeshatayarishwa. Jumla ya wajumbe 12 wameteuliwa na inatarajiwa kuzinduliwa rasmi kwa kuanza kazi mwezi huu wa Machi.

**b).** **Kufanya maandalizi ya mfumo wa majaribio ya mfumo wa kutathmini ufanisi wa utendaji wa kazi kwa ngazi ya kituo na Hospitali katika wilaya mbili kwa kuzingatia viashiria vya Afya.**

Kwa hatua ya awali, Wizara imeunda kamati ya wajumbe sita kutoka Idara ya Sera, Mipango na Utafiti na kuteua Afisa mmoja kutoka Divisheni ya Mipango na Maendeleo.Kamati kwa kushirikiana na watalamu elekezi wametengeneza muongozo utakaotumika katika kazi hii.Pia kamati imeweka viashiria (indicators) kwa ajili ya kupima ufanisi wa utendaji kazi katika vituo vya afya .Uhakiki umefanyika katika kituo cha afya cha Sebleni ambapo imeonekana kuwa viashiria vilivyopendekezwa vinaweza kutumika.

Kwa upande wa wilaya zilizopendekezwa ni Mkoani na Kaskazini A- Unguja.Vigezo vilivyotumiwa kuchagua wilaya hizo ni maradhi yaliyojitokeza pamoja na idadi ya watu.Hatua iliyofikiwa ni kufanya 'base line survey' kwa wilaya hizo.

c). **Kusimamia utekelezaji wa muongozo wa uchangiaji wa huduma za Afya.**

Muongozo wa kuchangia huduma za Afya umefanyiwa marekebisho kwa kutumia uzoefu wa nchi mbali mbali zilizoendesha mpango huo. Aidha gharama za kuchangia zilifanyiwa mapitio na kupangwa upya kulingana na gharama halisi za utoaji wa huduma za afya.

Muongozo huo umeshajadiliwa na kupitishwa katika kikao cha Kamati Tendaji kwa hatua ya utekelezaji. Kwa hivi sasa muongozo huo unasubiri kupata Baraka za Baraza la Mapinduzi. Hata hivyo, bado changamoto za uchangiaji wa huduma za afya zipo, hasa kwa upande wa msamaha (exemptions and waivers) ikiwemo wanawake wajawazito wanaojifungua kwa kawaida na kwa upasuaji.

**d). Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Afya ya Jamii (Community Health Strategy).**

Wizara tayari imewasilisha mkakati wa Afya ya Jamii Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ambao uko kwenye lugha ya kiingeraza kwa ajili ya kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili uweze kufahamika kwa wepesi zaidi kwa wahusika wakiwemo Kamati za Afya za Shehia. Hatua inayofuata ni kuuchapisha Mkakati huo ili usambazwe na kuanza kutumika rasmi. Kazi hii inatarajiwa kufanyika katika mwezi wa Machi, 2012.

e). **Kufanya ukarabati mkubwa wa majengo yaliyokuwa ya kiwanda cha sigara kwa ajili ya Bohari kuu ya dawa na Maabara ya Mkemia Mkuu.**

Ujenzi wa Bohari kuu ya dawa kwa sasa uko katika hatua ya kati. Jumla ya. shilingi milioni 62 kutoka serikalini zimeshatolewa ili kusaidia gharama za ujenzi huo ambazo zilitumika kwa ajili ya malipo ya umeme na maji. Kwa upande wa wafadhili tayari wameshaleta vifaa vya kukamilishia ujenzi huo. Wizara inatarajia kukabidhiwa rasmi jengo hilo mnamo mwezi wa Juni 2012. Kwa upande wa ukarabati kwa ajili ya maabara ya Mkemia mkuu, wizara tayari imeshaitisha kikao cha tenda ili kutafuta mkandarasi wa kufanya ukarabati huo.

f). **Kuchukua hatua za awali za kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya Rufaa.**

Katika kulifanikisha hili, wizara kwa kushirikiana na shirika la ICAP imefanya ukarabati mkubwa katika maabara ya Hospitali ya Mnazimmoja na kuifanya hospitali kuweza kufanya vipimo vingi.Ukarabati huo umefanya maabara hiyo kuwa na kiwango kizuri chenye kulingana na maabara nyengine zilizo ndani ya Afrika. Jumla ya shilingi milioni 300 zimetumika katika matengenezo hayo.

Wizara imesainiana mkataba na kampuni ya Orio ya Netherlands na itafanya matengenezo makubwa kwenye jengo la kiwanda cha dawa cha zamani. Hatua za awali zimeanza ikiwemo michoro ya jengo hilo litakavyokuwa.

Dental Unit ya Mnazi Mmoja nayo imefanyiwa ukarabati mkubwa pamoja na kuwekewa vifaa vipya vya kisasa kupitia ufadhili wa Miracle Corners of the World .Vile vile juhudi za uanzishwaji wa tiba kwa njia ya mawasiliano ya simu (Telemedicine) katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tayari imeshaanza.

Katika kuhakikisha Hospitali ya Rufaa kuwa na madaktari wa kutosha, wizara imehakikisha upatikanaji wa madaktari kwa kutiliana mkataba na Chuo kikuu cha Haukeland cha Norway ili kuleta madaktari bingwa kufanya kazi bega kwa bega na madaktari wazalendo.Vile vile madaktari wazalendo kutoka Mnazi mmoja nao hupata fursa ya kwenda Norway ili kufanya kazi katika hospitali za huko. Aidha kwa sasa hospitali hii inapokea madaktari bingwa kutoka Spain na Uholanzi kwa kutoa huduma za upasuaji wa mgongo na vichwa maji na madaktari kutoka Uholanzi wanafanya upasuaji wa plastic surgery.

Aidha kutakuwa na huduma za dialysis (matatizo ya figo) kwa wagonjwa, ambapo hatua iliyofikiwa ni kufanyika kwa "needs assessment" ambapo huduma hizi zinatarajiwa kupatikana hivi karibuni.

Kitengo cha wagonjwa mahututi kimeshaanza kufanyiwa hatua za awali za ukarabati kwa kupitia fedha za Serikali. Lakini hata hivyo kupitia Serikali ya Watu wa China wameahidi kujenga ICU nyengine mpya.

**g). Kuanza matayarisho ya kuzipandisha daraja Hospitali za Kivunge, Micheweni, vitongoji, Wete na Abdalla Mzee.**
**Hospitali ya Wete.**

Hatua za sasa zilizochukuliwa ni utanuzi wa majengo ya wodi ya wazazi ,watoto ,wanaume na wanawake yanayofanywa chini ya mkopo wa Benki ya Afrika.Pia wizara inaendelea na ujenzi wa sehemu ya matibabu ya wagonjwa wenye matatizo ya akili unaojumuisha Wodi mbili (ya wanaume na wanawake), sehemu 2 za matibabu na Afisi za wafanyakazi.

Pia kuna ujenzi unaoendelea wa sehemu ya tiba ya kazi kwa wale wanaoanza kupata nafuu (OT) au Occupational therapy. Ujenzi unasimamiwa na Mradi wa SMMRP – ADB. Aidha kuna ujenzi wa maabara mpya kwa msaada wa ICAP. Ujenzi huo utawezesha kuwa na sehemu tofauti za huduma za maabara pamoja na sehemu ya kutolea huduma kwa waathirika wa maradhi ya ukimwi (CTC).

**Hospital ya Abdalla Mzee Mkoani**

Wizara imeshafanya mazungumzo na Jamuhuri ya watu wa China na kukubali kuifanyia matengenezo makubwa na ya kisasa majengo yaliopo sambamba na Kujenga wodi mpya ya wazazi na wodi ya Watoto.

**Hospitali ya Micheweni**

Wizara imefanya utanuzi wa majengo ya wodi ya wazazi, matengenezo ya chuba cha upasuaji na ujenzi wa maabara mpya nay a kisasa.Pia wizara imweza kuipatia hospitali daktari mzoefu wa maradhi ya kinamama kutoka VSO kwa ajili ya kutoa huduma. Kwa upande wa hospitali ya vitongoji hatua bado hazijanza, lakini huduma zimeimarishwa kwa kuiongezea wafanyakazi wa kada mbali mbali kufikia daraja inayostahili.

**Hospitali ya kivunge**

Wizara imo kwenye mchakato wa kuongeza eneo na imeshafanya mazungumzo na wizara ya Kilimo na Maliasli kwaajili ya kuomba eneo lao lililopo pembeni ya hospitali hiyo wizara tayari imeshaoneshwa mipaka ya eneo na hatua iliyobaki ni ya makabidhiano tu, lengo la hatua hii ni kuzungusha uzio eneo lote ambapo kwa hivi sasa BOQ inatayarishwa kwa ajili ya kazi ya kuzungushwa uzio eneo hilo ili kwa hapo baadae tuweze kuongeza majengo.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI KATIKA BAADHI YA TAASISI ZA WIZARA

### 3.2.1 KITENGO CHA WAGONJWA MAHUTUTI (ICU)

Kamati katika ufuatiliaji wa shughuli za wizara ilitembelea pia Kitengo cha wagonjwa mahututi (ICU) katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.Kamati ilielezwa kuwa baada ya kumalizika kikao cha bajeti cha Baraza la Wawakilishi tarehe 6/08/2011 uongozi wa Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo zilifika hospitali ya Mnazi Mmoja na kuona hali halisi ya ICU.

Kufuatia ziara hiyo mapendekezo juu ya matengenezo yaliyotolewa na hatua za kusawazisha kasoro zilizobainika zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kuitisha zabuni.Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Afya iliwateuwa wakandarasi wawili walioshinda ambao ni kampuni ya **LAB EQUIP LTD** kwa ajili ya kuleta vifaa ambavyo vinagharimu shilingi milioni mia tatu(300,000,000/=) na kampuni ya **TOL GASES LTD** kwa ajili ya kusambaza bomba za hewa safi(centralized oxygen system) ambazo zitagharimu shilingi milioni mia mbili(200,000,000/=) .Mkandarasi wa **TOL GASES LIMITED** aliiomba wizara kumtangulizia asilimia 20 ya malipo sawa na Tsh. 59,910,046 na tayari wizara imefanya hivyo .Kampuni ya **LAB EQUIP LTD** imeahidi kukamilisha na kukabidhi kazi kwa Wizara ndipo apatiwe malipo yake yote kamili.Baada ya kufikia makubaliano hayo ,wakandarasi wote wameahidi kukamilisha kazi na kuikabidhi wizara kabla ya mwezi wa Julai 2012.

### 3.2.2 KITENGO CHA UKIMWI

**Fedha zilizopangwa kutoka SMZ Tsh 297, 724,000/=**

**Fedha zilizotolewa July-Disemba Tsh 11,846,000/**

**Fedha zilizopangwa kutoka msaada wahisani Tsh 4,014,983,000/=**

**Fedha zilizotolewa kutoka wahisani: ICAP –Tsh. 145,314,117/=, CDC/GF- $2,430,509.52/=**

**Utekelezaji**

Kitengo cha Ukimwi kinafanyakazi kupitia maeneo yake makuu matatu:

- Mafunzo kwa wafanyakazi wa Afya
- Huduma kwa jamii
- Ufuatiliaji wa kazi

Kwa kipindi cha Julai –Disemba kitengo kilifanya kazi zake kupitia:-

- Huduma kwa jamii

Jumla ya wagonjwa 5,923 wamesajiliwa katika kliniki zao .Wagonjwa 3172 sawa na asilimia 54 wanatumia dawa za ARVsmiongoni mwao 303 sawa na asilimia 10 ni watoto.

Jumla ya watu 32,284 walichunguzwa katika vituo 53 vya ushauri nasaha na upimaji virusi vya Ukimwi (vvu)kwa hiari,vikiwemo vituo vya serikali na binafsi.Wanawake 15,412 na wanaume 16,872.Pia upimaji katika vituo vya dharura (out reach), wanawake walikuwa 343 na wanaume ni 206 na kufanya idadi ya 549.

Katika kujikinga na maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, jumla ya wajawazito 10,288 walichunguzwa VVV katika Kliniki na wodi ya wazazi kati yao wajawazito 52 waligundilikana na VVUna kupatiwa dawa za kinga.

Katika kuboresha huduma za tiba katika maabara, kitengo kilipokea CD4 mashine moja mpya ambayo imepelekwa katika hospitali ya Mwembeladu na mashine ya Heamatology na Chemistry" ambazo zimepelekwa katika hospitali ya Micheweni, Makunduchi na Mwembeladu.

**Changamoto:**

- Uhamisho wa wafanyakazi na uhaba wa wafanayakazi na majukumu mengi waliokuwanayo wafanyakazi wa vituo vya afya ambayo yanaathiri ufanisi wa utoaji wa huduma endapo zitaanzishwa.
- Baadhi ya watoa huduma wanahitaji mafunzo ya muda mrefu ya ushauri nasaha pamoja na mafunzo msasa.
- Uhamisho wa wafanyakazi walikwishapata mafunzo katika vitu vyao.
- Kutokubalika kwa mipira ya baba/mama katika jamii kutokana na kuwepo kwa dhana potofu dhidi ya mipira hiyo lakini kitengo kinaendelea na mikakati ya kuelimisha jamii kuhusiana na hali hiyo hasa katika taasisi za kidini.

### 3.2.3 KITENGO CHA MALARIA

**Utekelezaji wa malengo**

- **Kuendeleza kugawa vyandarua katika kaya kwa nchi nzima**

Kitengo cha Malaria kwa kushirikiana na washirika wa Maendeleo,kinaendelea na utaratibu wa kugawa vyandarua vyenye dawa ya muda mrefukwa nchi nzima bila ya malipo kwa wastani wa vyandarua vitatu kwa nyumba moja . Kiasi ya vyandarua elfu saba vinategemewa kusambazwa Unguja na Pemba .Kitengo kimesajili nyumba na wakaazi wote ili kupata idadi halisi inayohitajika kwa kila Kaya .

- **Uzinduzi wa usimamizi wa uuzaji wa dawa za Malaria kwa bei nafuu.**

Utekelezaji wake ni baina ya kitengo na mwekezaji binafsi katika sekta ya dawa Izmir Pharmacy ya Darajani Mjini Unguja. Jumla ya dozi 150,000 za dawa mchanganyiko kwa matumizi ya umri mbali mbali zimenunuliwa na muwekezaji huyo kwa iliyopangwa na Serikali kupitia Wizaya ya Afya .Wauzaji wa aina tofauti wanauza kwa wananchi kwa bei ya chini ya Tsh.500 kwa dozi ya watoto wachanga na bei isiyozidi 1000 kwa watu wazima .Hii ni bei punguzo kwa asilimia zaidi ya 600 kutoka kwenye bei iliyozoeleka awali kuanzia shilingi 6500 hadi shilingi 14000 kwa dawa za aina hii kwenye maduka binafsi Unguja na Pemba.

**Changamoto**

- Uhaba wa fedha zinazotolewa na serikali
- Kitengo kutegemea zaidi asilimia 98 ya fedha za wafadhili
- Wananchi kulegeza mikakati ya kujikinga na kupambana na malaria
- Kujitokeza kwa dalili za usugu wa mbu kwa dawa zinazotumika kuwauwa.

### 3.2.4 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA YA AFYA KWA UPANDE WA PEMBA

**UTEKELEZAJI HALISI**

a). **Kuwapatia mafunzo ya ndani na nje Wafanyakazi wa kada za Utawala na Uendeshaji**

Jumla ya wafanyakazi 48 wako masomoni kwa kipindi cha Julai – Septemba 2011/2012, kati yao wanawake 20 na wanaume 28.Wafanyakazi waliorudi masomoni ni wanane (8) ,wanaume 7 na mwanamke 1, ambao wote wameshapangiwa kazi. Kada za waliorudi masomoni ni kama vile: Vector 5, wanaume 4 na mwanamke 1, mafundi 2 wanaume.

Jumla ya vijana 78 wakiwemo wanaume 43 na wanawake 35 wamepatiwa nafasi za kujiunga na Chuo cha Afya Mbweni kwa kuanza masomo ya Afya kwa mwaka 2011/2012.

b). **Ujenzi wa Maabara ya Hospitali ya Chake-Chake - Pemba**

Ujenzi wa Maabara hii umekamilika na maabara tayari imeanza kazi kuanzia Januari. Ujenzi umegharamiwa kwa Msaada wa ICAP

c). **Upimaji wa Maeneo.**

Upimaji wa Maeneo ya Programu ya RCH, EPI, ZACP na Elimu ya Afya Machomane na MCH kliniki umefanyika, kilichobaki ni kukamilisha Site Plan kwa ajili ya kulipia gharama za Waraka wa kumiliki maeneo hayo.

d). **Kwa upande wa miradi ya Ujenzi wa Vituo vya Afya vinavyojengwa na wananchi**,

Wizara husaidiana na wananchi husika katika hatua za awali zikiwemo kuwapatia ramani ya jengo na utaalamu kwa kumshirikisha fundi Mkuu wa Wizara kuona kwamba ujenzi unaofanywa unazingatia vigezo vya Wizara vilivyowekwa.Vituo vilivyojengwa na wananchi kama ifuatavyo: - Wilaya **ya Micheweni -** Chimba, Kifundi, Ungi, **Wilaya ya Wete-**Mjini Kiuyu, Bwagamoyo, Mtambwe, **Wilaya ya Chake Chake -** Mbuzini, Vikunguni, Kibokoni, Vitongoji, Matale na Chanjamjawiri, **Wilaya ya Mkoani -** Tasini Kiwani.

### 3.2.5 UTEKELEZAJI WA BAJETI KATIKA BAADHI YA TAASISI MAALUM

### 3.2.6 BOHARI KUU YA DAWA PEMBA

Kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2011 Bohari kuu ya dawa iliweza kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kupokea na kusambaza dawa na vifaa vya tiba katika Hospitali na vituo vya afya vyenye thamani ya shilingi 84,860,400 kati ya hizo shilingi 50,415,500 ni dawa zilizo katika mfumo wa **bulk** na shilingi 34,444,900 ni dawa zilizo katika mfumo wa **kit** na hupelekwa katika vituo vya afya.
- Kitengo kimeweza kutoa mafunzo juu ya usimamizi wa matumizi sahihi ya dawa kwa wahudumu 15 kutoka vituo vya afya Chake Chake hospitali.

### 3.2.7 MKEMIA MKUU WA SERIKALI PEMBA

Idara ya Mkemia Pemba imeweza kupokea jumla ya vielelezo 24 vyenye aina mbali mbali za sampuli katika kipindi cha Julai/Septemba kutoka Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi. Aina za sampuli hizo zikiwemo madawa ya kulevya, ulevi wa kienyeji na zile za mkojo kuchunguza watumiaji wa dawa za kulevya.

## 4.0 MAONI YAKAMATI

- Kamati inaitahadharisha serikali kukifanyia mapitio na kutafuta namna ya kukiimarisha Chuo cha madaktari cha Zanzibar ili kiweze kutoa madaktari wenye uwezo kitaaluma na kusaidia sekta ya afya nchini. Chuo hichi kina umuhimu wa aina yake kwa vile ni tegemeo la madaktari wazalendo wa baadae.Eneo la Chuo linalotumika hivi sasa ni dogo sana kiasi ambacho ni vigumu kuweza kuchukua wanafunzi wengine (new intake) kutokana na upungufu wa majengo.Kwa mfano kwa upande wa Unguja,kuna madarasa mawili tu ambayo kwa sasa yanatumika kwa wanafunzi waliopo. Aidha Kamati imebaini kuwa miongoni mwa eneo jengine la msingi ambalo kuna haja kwa Serikali kulizingatia ni Ukosefu wa wafadhili katika Mradi wa Chuo, hali ambayo hupelekea Chuo kutegemea fedha za serikali tu ambazo kwa kweli hazitoshelezi.

- Kamati imeridhika na hatua ya maendeleo ya Mradi wa ujenzi wa **Bohari kuu ya dawa Zanzibar** chini ya washirika wa maendeleo USAID na DANIDA pamoja na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali imechangia jumla ya shilingi milioni mia moja kati ya shilingi milioni mia mbili zilizopangwa kutolewa.Jumla ya shilingi bilioni moja nukta mbili zimepangwa kutumika katika mradi huu ambao unatarajiwa kumalizika mwezi Mei 2012 na kukabidhiwa Juni 2012**.** Kamati inaisisitiza wizara kuendelea kuimarisha ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa ujenzi huo unamalizika kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

- Katika kufanikisha juhudi za mapambano dhidi ya maradhi ya ukimwi, kamati imeona ipo haja kwa Wizara ya Afya kuvishauri vituo vya afya vya binafsi kuwa tayari kupeleka wauguzi wao kupata mafunzo ya "nurse assistance" ili waweze kusaidia katika utoaji wa huduma za dawa za ARV kwa mujibu wa utaratibu wa Kitengo cha huduma za maradhi ya ukimwi.

- Kamati inakipongeza kitengo cha kupambana na malaria katika juhudi za kutokomeza malaria nchini.Hata hivyo imekishauri kitengo hicho kujenga hoja za kitaalamu ili kuweza kupatikana dawa mbadala na mchanganyiko ambazo zitaua mbu wanaosababisha malaria na maradhi mengine.

- Kwa kuwa Wizara imekamilisha muongozo wa tathmini wa kubaini mapungufu katika ngazi ya hospitali za wilaya na vijiji(cottage hospitals),Kamati inaishauri serikali kuzitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto za msingi zinazozikabili hospitali nyingi za wilaya na vijiji Unguja na Pemba, ili kusaidia upatikanaji wa huduma za msingi za afya katika maeneo hayo.

- Kamati inakipongeza Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kwa kuwa na ubunifu endelevu kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya chuo hicho.Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kuwa na mpango wa kuanzisha utoaji wa mafunzo ya afya kupitia mtandao "e- learning" chini ya msaada wa wataalamu kutoka Uingereza na Ujerumani, kufikiria juu ya ujenzi wa uzio pamoja na kuzishauri taasisi binafsi ili kusaidia kuwapatia mikopo wanafunzi wa Diploma wa Chuo.

  Chuo kimeweza kuanzisha utaratibu mpya wa teknolojia ya kisasa kupitia "website" ambao utatumiwa na wanafunzi wakati wa kujiunga na Chuo.

  Chuo kimeanzisha ujenzi wa jengo jipya la Elimu ya juu pamoja na dakhalia 2 za wanawake ikiwa ni msaada kutoka serikali ya Oman.

- Mchango wa Fedha za serikali katika maeneo mengi ya sekta ya afya katika utekelezaji wa miradi bado ni mdogo ukilinganisha na makisio yaliyopangwa.Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi katika kuhakikisha kuwa inachangia ipasavyo ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo.

- Kamati inaishauri serikali kuijengea uwezo zaidi sekretarieti inayosimamia mabadiliko ya sekta ya afya Zanzibar ili iweze kukabiliana na changamoto za mahitaji ya msaada wa ushauri wa kitaalamu kutoka taasisi za kimataifa ambao umeonekana kuwa na gharama kubwa.

### 4.1 MAAGIZO YA KAMATI

- Kamati imeiagiza Wizara kuharakisha kuanza ujenzi wa jengo la ofisi za Mkemia Mkuu wa Serikali ili chombo hicho muhimu kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

- Kwa kuwa Wizara imekamilisha muongozo wa tathmini wa kubaini mapungufu katika ngazi ya hospitali za wilaya na vijiji(cottage hospitals),Kamati imeitaka wizara kufuatilia na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto za msingi zinazozikabili hospitali nyingi za wilaya na vijiji Unguja na Pemba, ili kusaidia upatikaji wa huduma za msingi za afya katika maeneo hayo.Miongoni mwa

changamoto hizo ni tatizo la upungufu na ukosefu wa huduma ya maji safi ,baadhi ya dawa muhimu(kama za mama wajawazito),upungufu wa wauguzi na madaktari,pamoja na vifaa muhimu n.k.

- Kamati imebaini kuwa hakuna uhakika wa upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa wa akili, hivyo inaiagiza wizara kuzingatia upatikanaji wa dawa hizo ili ziweze kusaidia katika matibabu ya afya ya akili.

- Kamati inaiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa inashirikiana na Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya katika kukipatia ruzuku chuo hicho kama vinavyopatiwa vyuo vyengine ili kiweze kuongeza ufanisi kwa lengo la kuimarisha sekta ya afya nchini.

### 4.1.1 HITIMISHO

Kamati hairidhiki kuwepo kwa mchango mdogo wa fedha za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikilinganishwa na makisio yaliyopangwa. Iwapo serikali itaendelea na utaratibu huu kuna uwezekano wa kukosekana kwa ufanisi katika sekta muhimu ya afya.

## 5.0 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

### 5.1 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA RIPOTI YA KAMATI KWA MWAKA 2010/2011

- **Kamati imeiagiza Wizara kuhakikisha kuwa malengo ya Ujenzi wa Mradi wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) yanatekelezwa ipasavyo ili chuo hicho kiweze kutumika kabla ya Septemba 2011.**

Katika mwaka wa fedha 2011/12, Serikali imejitahidi kuingiza fedha ili kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika ifikapo Disemba 2011. Ujenzi umo katika hatua za mwisho kwa majengo ya utawala, maktaba na kitivo cha Elimu (sanaa na sayansi). Kwa upande wa kitivo cha uhandisi, ujenzi umefikia asilimia 85. Wizara inatarajia kukabidhiwa majengo hayo mnamo mwezi wa Juni, 2012.

- **Wizara imeagizwa kufuata sheria ya kazi ya kuwapatia likizo la walimu kila mwaka pamoja na maposho yao badala ya kuendelea na mfumo uliopo sasa wa kuwapatia maposho walimu hao kila baada ya miaka mitatu.**

Wizara bado haijatekeleza agizo la kuwapatia likizo walimu kila mwaka pamoja na maposho yao. Utaratibu uliopo ni kuwa wafanyakazi watapata likizo kila mwaka baada ya kuomba. Sababu ya kufanya hivyo ni kwamba kanuni za GO (General order) inayotumika sasa inataka wafanyakazi wapewe posho la likizo kila baada ya miaka mitatu na siyo kila mwaka kama kamati ilivyoagiza.

Utaratibu wa kuwapatia posho la likizo wafanyakazi, hili limeamuliwa na Serikali kuu kuwa kila mfanyakazi mwenye likizo atapata posho la Tsh. 100,000/- kila baada ya miaka mitatu badala ya Tsh 30,000/- waliyokuwa wakipatiwa hapo zamani. Utekelezaji huu wa kuwapatia posho la Tsh. 100,000/- tayari umeshaanza kutekelezwa.

Hata hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeandaa mpango maalum kwa wafanyakazi ambao wanakwenda likizo. Mpango wenyewe ni kwamba $^{1}/_{3}$ ya wafanyakazi wa Wizara wataruhusiwa kwenda likizo na kupewa posho kwa kila mwaka. Sababu ya kupanga hivyo ni kwamba wafanyakazi wengine 2/3 wabakie kazini ili shughuli nyengine za kazi ziendelee kama kawaida.

- **Kamati haikuridhika na idadi ya skuli zilizofanyiwa ukaguzi, hivyo imeagiza Wizara kuhakikisha kuwa dosari hiyo inaondoshwa.**

Idadi ya skuli zinazokaguliwa kwa mwaka hupangwa na kuandikwa kwenye kamusi la utekelezaji, ambalo hutayarishwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu. Idadi hiyo inategemea mambo yafuatayo:-

- Idadi ya wakaguzi waliopo.
- Kalenda ya ufunguaji na ufungaji wa skuli kwa mwaka mzima.
- Kuingiliwa siku za masomo na mambo mbali mbali, kama sherehe za kitaifa na kiwizara, mitihani ya skuli, mitihani ya pamoja kikanda, kiwilaya, kimkoa na kitaifa, (yaani F II, FIV, FVI)

Kwa kuzingatia hayo, idadi ya skuli zilizopangiwa kukaguliwa kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama ifuatavyo:-

| S/N | MWAKA | LENGO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | 2009/2010 | 160 | 166 |
| 2. | 2010/2011 | 180 | 213 |
| 3. | 2011/2012 | 190 | 131 (Dec) |

Dosari hiyo inaondoshwa kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuzidisha idadi ya skuli zinazokaguliwa kila mwaka kwa kiasi kinachowezekana na kujitahidi kuvuka lengo hilo.
- Kuipatia nyenzo Ofisi ya Mkaguzi Mkuu ili kuweza kutekeleza jukumu hilo.
- Kuchagua wakaguzi wengine kuziba pengo la wakaguzi wanaostaafu au kuhama kikazi.
- Mipango ya baadae ni kuwepo na wakaguzi wa Wilaya Unguja na Pemba.

- **Kamati imeagiza Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ithibitishe Ripoti za Ukaguzi za Walimu Wakuu kabla ya kuziwasilisha Wizarani.**

Utaratibu ambao unatumika na ambao unategemewa kuleta ufanisi kwa skuli ni:-

- Kuzipitia ripoti za walimu wakuu na kutoa maoni na maelekezo kwa skuli hizo.
- Baadae Mkurugenzi anayehusika na skuli naye huzipitia na kutoa maoni yake kwa skuli.
- Katibu Mkuu naye huzipitia na kutoa maoni yake, pamoja na maelekezo zaidi.

Usahihi wa ripoti, na marekebisho zaidi hutokea pale ambapo ukaguzi kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu hufanyika katika skuli hizo.

Madhumuni hasa ya ukaguzi wote huo ni kuleta ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji kwenye skuli hizi.

**5.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA YA WANANCHI JULAI/ DISEMBA, 2011**

**MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA MAANDALIZI**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh. 200,000,000/=, UNICEF $307,000,000/=**

**Lengo: Kukamilisha ujenzi wa skuli mbili za maandalizi Unguja na Pemba**

Ujenzi wa skuli ya Maandalizi Potoa na Ungwi Micheweni umekamilika kwa hatua zote bado kuvuta umeme na kuingiza samani.

Maandalizi ya zabuni kwa ajili ya ununuzi wa samani za skuli za Potoa na Ungwi umeanza fedha zilizopatikana kwa ajili hiyo ni Tsh. 40,000,000/= kutoka SMZ.

**Lengo: kutayarisha Sera ya makuzi, malezi na maendeleo ya mtoto**

Mafunzo ya awali ya utayarishaji wa Sera ya makuzi, malezi na maendeleo ya mtoto yametolewa kwa wasimamizi wa "ECD RESOURCE PARK" .Fedha zilizopatikana ni Tsh. 23,859,300/= kutoka UNICEF.

**Lengo: Kuendeleza kutoa mafunzo ya mtaala mpya kwa walimu wa skuli za maandalizi.**

Mtaala mpya wa elimu kwa walimu wa maandalizi umefanyiwa mapitio na kuhaririwa .Jumla ya Tsh. 10,000,000/= zimepatikana kutoka SMZ.

**MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA MSINGI**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh. 1,000,000,000=/, CHINA Tsh. 2,250,000,000/=, SIDA, USAID na**

**UNICEF Tsh. 4,969,938,000/=.**

**Lengo: Kukamilisha ujenzi wa madarasa 200 yaliyoanzishwa na wananchi Unguja na Pemba**

Ujenzi wa madarasa (kwa hatua za kuezeka plasta,sakafu na rangi) katika skuli za Magogoni(6),Mwanakwerekwe D/G (2),Mto wa Pwani (6),Donge Karange (6),Mangapwani (5),Mtopepo(3),Maziwang'ombe (4),Kinowe(3),Ungwi(3) na Ukutini (4) umekamilika .Fedha zilizopatikana ni Tsh. 238,000,000/= kutoka SMZ.

**Lengo: Kuzifanyia ukarabati skuli 15 Unguja na Pemba**

Skuli zilizofanyiwa ukarabati ni Mkunazini, Donge msingi, Kiboje, Muembe Makumbi, Minungwini na Michenzani.Fedha zilizopatikana kwa kazi hiyo ni Tsh. 32,000,000/= za SMZ.

**Lengo: Kuzipatia samani skuli mbali mbali Unguja na Pemba**

Uchongaji na usambazaji wa madawati umefanyika kwa skuli za msingi za Welezo (45),Magogoni(60),Mtoni(45),Mwera(90),Jumbi(60),Cheju(90),Ubago(60),Chambani(75),Ukutini(105),Mgelema(45), Mkanyageni(75),Madungu(75).Fedha zilizopatikana ni Tsh.103,765,800 kutoka SIDA.

Uchongaji wa madawati 345 kwa skuli za msingi za mikoa ya kaskazini Unguja na 345 kaskazini Pemba unaendelea.

**MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA UFUNDI**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh.400, 000,000/=**

**Lengo: Kukamilisha ujenzi wa madarasa 4 mapya katika skuli ya Sekondari Kengeja**

Ujenzi wa madarasa 4 umekamilika.Fedha zilizotumika ni Tsh.10, 000,000/=

**MRADI WA UPANUZI NA UIMARISHAJI WA HUDUMA ZA MAKTABA**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh.150, 000,000/=**

**Lengo: Kuanza Ujenzi wa Maktaba kuu Pemba**

Matayarisho ya ujenzi wa maktaba kuu tawi la Pemba yameanza kwa hatua ya usafishaji wa eneo.Fedha zilizopatikana ni Tsh.100, 000,000/= kutoka SMZ.

**MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU MBADALA NA AMALI**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh.150, 000,000/=, ADB Tsh.3, 000,000,000/=**

**Lengo: Kukamilisha ujenzi wa kituo cha elimu mbadala Wingwi Mtemani**

Kazi za ujenzi zimeendelea kwa hatua za kupiga plasta ndani na nje ya jengo.

**Lengo: Kununua samani na vifaa vya kufundishia.**

Maandalizi ya zabuni kwa ajili ya vifaa husika yameanza.

**Lengo: Kuanza utekelezaji wa mradi wa ALSD II**

Mkataba kwa ajili ya kupatiwa mkopo wa kutekeleza mradi wa elimu mbadala na amali awamu ya 2 umetiwa saini baina ya ADB na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania

**MRADI WA UKAMILISHAJI WA UJENZI WA MAKAO MAKUU YA WIZARA**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh.25, 000,000/=**

**Lengo: Kutayarisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la pili la Wizara.**

Rasimu ya awali ya michoro husika imetayarishwa na ukarabati wa baadhi ya ofisi za wizara umefanyika.Fedha zilizopatikana ni Tsh. 7,000,000/= za SMZ.

**MRADI WA UKAMILISHAJI WA UIMARISHAJI WA CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh. 1,725,000,000/=, BADEA Tsh. 438,000,000/=**

**Fedha zilizopatikana kutoka SMZ Tsh. 700,000,000/=, $ 143, 024, 91/= kutoka BADEA.**

**Lengo: Kukamilisha Ujenzi wa majengo manne ya Chuo.**

Ujenzi wa majengo manne ya chuo unaendelea kwa hatua za milango, madirisha na makabati na mabenchi ya maabara.

**Lengo: Kununua vifaa vya maabara na samani**

Mkataba kwa ajili ya ununuzi wa samani na vifaa vya maabara umetiwa saini baina ya wizara na wazabuni wahusika. Wazabuni hao kwa upande wa samani ni QUALITY FURNITURES NA GENERAL APPLIANCES ambapo vifaa hivyo vilikuwa vinatarajiwa kukabidhiwa Februari 2012.Kwa upande wa vifaa vya maabara, ni kampuni ya BIOLOGY MFI OFFICE SOLUTIONS, PHYSICS ALTERNATIVE SOLUTIONS NA CHEMISTRY, hao pia wizara ilikuwa inasubiria “no objection” kutoka BADEA ili kupatikana kampuni itakayoonekana inafaa.

**Lengo: Kununua na kufunga vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

Zabuni kwa ajili ya vifaa hivyo imetangazwa.

**MRADI WA UKAMILISHAJI WA ELIMU YA LAZIMA**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh. 900,000,000/=, Benki ya Dunia Tsh. 40,500,000,000/=, BADEA Tsh. 3,930,054,000/=**

**Lengo: Kununua baadhi ya vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa madarasa ya Sekondari.**

Wizara imetiliana saini mikataba na wazabuni wa vitabu husika.

**Lengo: Kuchonga seti 20750 za meza na viti kwa wanafunzi wa Skuli za Sekondari**

Zabuni kwa ajili ya uchongaji wa samani zimetangazwa, zimeuzwa, zimefunguliwa na zimefanyiwa tathmini.Mikataba na wazabuni husika imetiwa saini. Fedha zilizopatikana kwa shughuli hiyo ni Tsh 20,177,572 kutoka Benki ya Dunia. Seti 500 za meza na viti zimechongwa na kusambazwa katika Skuli za Sekondari za Fuoni, Mtopepo, Mtende, na Pale.Fedha zilizopatikana ni Tsh.60, 000,000 kutoka SMZ.

**Lengo: Kukamilisha Ujenzi wa Skuli 16 Unguja na Pemba.**

Ujenzi unaendelea vizuri kwa hatua tofauti katika skuli 13 isipokuwa skuli 3 za Paje Mtule, Tunguu na Dimani. Fedha zilizotumika ni Tsh. 1,925,853,231.95/=.

**Lengo: Kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Willium Mkapa Mchangamdogo Pemba.**

Ujenzi unaendelea kwa hatua za madirisha, milango, dari, mfumo wa maji safi na maji machafu, Fedha zilizopatikana kutoka Benki ya Dunia ni Tsh. 262,183,364/=

**Lengo: Kuendelea na ukarabati wa Skuli 6 za sekondari**

Skuli zilizofanyiwa matengenezo hayo kwa hatua mbali mbali ni Skuli ya Fidel Castro, Utaani, Forodhani na Tumekuja.Fedha zilizopatikana katika matengenezo hayo ni Tsh. 834,992,775.4/=

**Lengo: Kuanza ujenzi wa Skuli za Sekondari za ghorofa za Kiembesamaki, Mpendae na Kwamtipura**

Zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi zimetangazwa na wizara inasubiri “no objection” kutoka Benki ya

Dunia.Fedha zilizopatikana ni Tsh. 24,182,000/=

**Lengo: Kuanza ujenzi wa Skuli za Sekondari za ghorofa za Kibuteni na Mkanyageni**

Zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi zimetangazwa na wizara inasubiri “no objection” kutoka BADEA .Fedha zilizopatikana ni Tsh. 11,430,000/= kutoka SMZ.

**MRADI WA CHUO CHA KIISLAM MICHEWENI PEMBA**

**FEDHA ZILIZOTENGWA: SMZ Tsh. 50,000,000/=**

**Lengo: Kujenga uzio katika eneo la Chuo.**

Ufyatuaji wa matofali kwa ajili ya ujenzi huo umeanza. Fedha zilizotumika ni Tsh 15,000,000/= za SMZ.

**5.3 UTEKELEZAJI WA MATUMIZI YA FEDHA.**

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilipanga kutumia Tshs 4,500,000,000 kwa kazi za maendeleo na Tshs 36,490,584,000 kwa kazi za kawaida.

Katika kipindi cha Julai – Disemba, Wizara imepatiwa jumla ya Tshs 1,650,000,000 kwa kazi za maendeleo na Tshs 21,015,281,188 kwa kazi za kawaida.

Kwa upande wa mapato, Wizara ilikusanya Tshs 3,423,600 kupitia vyanzo vya leseni za walimu na leseni za miradi.

**5.4 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

Katika kipindi cha nusu mwaka julai/disemba 2011/2012, utekelezaji halisi wa malengo ya bajeti ya Wizara ilikuwa kama ifuatavyo:-

**Lengo: Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufundishia**

Wizara kwa kupitia Mradi wa ICT “21 Century Basic Education” imeanza kuchukua hatua za kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufundishia na kujifunzia. Katika kipindi cha Julai – Disemba 2011 shughuli zifuatazo zilifanyika.

- Kumefanywa utafiti Unguja na Pemba kwa walimu wa darasa la kwanza hadi la nne wanaosomesha masomo ya Hisabati, Kiswahili, Sayansi na Kiingereza zilizolenga kujua mada zinazowapa tabu walimu katika ufundishaji wake.
- Skuli 2 za majaribio (Darajani na Kisiwandui) pamoja na Kituo kimoja cha Ualimu (Michakaini) vimewekewa vifaa vya ICT.
- Utayarishaji wa “e-content” umeanza.
- Dodoso za kukusanyia takwimu mbali mbali za skuli zimetayarishwa.

**Lengo: Kuimarisha Utoaji WA Mafunzo ya Walimu katika Vyuo Na Vituo vya Walimu**

- Wakufunzi wa Vyuo na Vituo vya Walimu walipatiwa mafunzo yenye lengo la kuongeza uwezo wao kwa kufundisha lugha ya Kiingereza na Mawasiliano kwa walimu wa Sekondari.
- Wakufunzi watano wa masomo ya Sayansi na Hisabati walipatiwa mafunzo ya ufundishaji bora wa masomo hayo nchini Kenya baada ya kuhudhuria na kushiriki katika warsha hiyo.

**Lengo: Kutoa Mafunzo kwa Walimu wa Maandalizi juu ya mbinu bora za Ufundishaji kwa kupitia Redio na Vituo vya Walimu**

Moduli za masomo kwa ajili ya mafunzo ya walimu kwa njia ya redio zimetayarishwa. Mafunzo haya yanategemewa kuanza kutolewa mwezi wa Machi 2012.

**Lengo: Kutoa mafunzo kwa walimu 360 wa msingi katika lugha ya Kiingereza na masomo ya Sayansi na Hesabati**

Mafunzo ya lugha ya Kiingereza, Sayansi na Hisabati yametolewa kwa walimu 360 (wanawake 184 na Wanaume 176)

wanaofundisha Kiingereza, Sayansi na Hisabati katika skuli za msingi. Mafunzo haya yaliendeshwa katika vituo vyote vya walimu 9 Unguja na Pemba katika mwezi wa Novemba na Disemba 2011.

**Lengo: Kufanya tafiti mbali mbali za kielimu**

- Ripoti ya Utafiti wa SACMEQ III imekamilika na imewasilishwa International Institute of Educational Planning (IIEP) Paris, Ufaransa.
- Matayarisho ya vipeperushi kwa ajili ya kuwasilisha matokeo ya utafiti wa SACMEQ III kwa walimu yamekamilika.
- Maandalizi ya awali (concept note) ya tathmini ya Elimu kwa Wote yameshakamilika na yameshawasilishwa UNESCO kwa ajili ya kupatiwa fedha.
- Hatua ya awali ya kutayarisha "project proposal" kwa ajili ya utafiti kuhusiana na ubora wa mbinu zinazotumika kutahini wanafunzi katika ngazi ya elimu ya lazima imekamilika.
- "Concept note" kwa ajili ya zoezi la "literacy survey" imeshatayarishwa na kuwasilishwa UNESCO kwa ajili ya kupatiwa fedha.

**Lengo: Kuandika, kuchapisha na kusambaza vitabu vya wanafunzi na viongozi vya walimu kwa madarasa ya I- III**

Vigezo kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya msingi (darasa la I hadi IV) kwa masomo ya Sayansi, Hisabati, Sayansi Jamii na Kiingereza vimetayarishwa. Vitabu hivi vitanunuliwa kupitia mradi wa Elimu ya lazima unaogharamiwa na Benki ya Dunia

**Lengo: Kuupitia na kuurekebisha mtaala wa Diploma ya Ualimu Msingi**

Rasimu ya awali ya mtaala wa Diploma ya Ualimu Msingi imeandaliwa. Mshauri muelekezi anakamilisha kazi husika.

**Lengo: Kuandikisha wanafunzi katika ngazi ya maandalizi**

Jumla ya wanafunzi 3,084 (1,560 wavulana na 1,524 wasichana) wameandikishwa kuanza elimu ya maandalizi katika Skuli za Serikali Unguja (1,716) na Pemba (1,368).

**Lengo: Kuandikisha wanafunzi katika ngazi ya Elimu ya msingi**

Jumla ya wanafunzi 22,354 (11,170 wavulana na 11,184 wasichana) wameandikishwa kuanza elimu ya msingi katika Skuli za Serikali Unguja (13,491) na Pemba (8,863).

**Lengo: Kuzikagua skuli 190 zikiwemo skuli 140 za Serikali na 50 za binafsi**

Jumla ya skuli 131 zimekaguliwa. Kati ya hizo 11 ukaguzi mkuu, 40 ukaguzi wa ziara, 23 ukaguzi maalum, 46 ukaguzi wa ufuatiliaji, na 11 ukaguzi wa usajili.

**Lengo: Kudhamini wanafunzi wapya 250 wa elimu ya juu**

Jumla ya wanafunzi 209 wapya wa fani mbali mbali wamedhaminiwa kujiunga na masomo katika Vyuo mbali mbali vya Tanzania.

**Lengo: Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na SUZA**

Chuo Kikuu cha SUZA kimeandikisha wanafunzi wapya 533 kwa mwaka wa masomo 2011/12 katika kozi zifuatazo :-

- Cheti cha Kompyuta - 18
- Diploma ya Elimu, Utawala na Uongozi - 40
- Cheti cha IT - 26
- Diploma ya IT - 36
- Diploma ya Sayansi na Ualimu - 34

- Diploma ya Kompyuta - 22
- Diploma ya Lugha - 168
- Diploma ya Kompyuta - 15
- Shahada ya Ualimu (Sayansi) - 47
- Shahada ya Ualimu (Sanaa) - 163

Hadi Disemba 2011, Chuo kilikuwa na jumla ya wanachuo 1,441 ikilinganishwa na 1,224 wa mwaka 2010/2011

**Lengo: Kutoa na kusimamia mafunzo ya Amali kwa vijana 600 katika vituo mbali mbali vya Mafunzo ya Amali**

Jumla ya vijana 587 (wanawake 139) wanapata mafunzo ya amali katika vituo vya Mafunzo ya Amali vya Mkokotoni, Vitongoji na Mwanakwerekwe.

**Lengo: Kusajili upya vituo vyote vinavyotoa mafunzo ya Amali Unguja na Pemba**

Kati ya vituo sita vilivyopangiwa ukaguzi, vitano kati yao vimetimiza sifa za kusajiliwa. Vituo vilivyokaguliwa ni :-

- Zanzibar Professional Training College.
- Hamoup Hotel and Catering Institute
- Smart Institute of Business and Technology
- Dar – es – salaam College of Hotel and Business Studies.
- The East African Utalii College.

NB: Kituo cha “Zanzibar School of Health” hakikukidhi sifa za kukaguliwa.

**Lengo: Kutayarisha Sheria ya uanzishaji wa Bodi ya Upimaji Na Tathmini**

Rasimu ya awali ya sheria imetayarishwa. Rasimu hiyo inapelekwa katika vikao husika kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

**Lengo: Kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani ya Taifa ya darasa la saba na kidato cha pili**

Mitihani ya Taifa ya darasa la saba na kidato cha pili imetungwa, imesimamiwa na imesahihishwa. Jumla ya wanafunzi 23,798 (wasichana 12,555 na wavulana 11,243) wa darasa la saba na 19,665 (wasichana 10,546 na wavulana 9119) wamefanya mitihani hiyo.

**Lengo: Kufungua vituo vya kujiendeleza kila inapohitajika.**

Vituo vipya viwili vya kujiendeleza vimefunguliwa katika maeneo ya Mfenesini na Kinyasini (Unguja).

**Lengo: Kufungua madarasa ya kisomo kila ambapo wananchi watajitokeza**

Jumla ya madarasa saba ya kisomo yamefunguliwa. Matano katika vijiji vya Kijini na Mbuyutende, moja kijiji cha Kitumba na moja kijiji cha Mgeni Haji.

**Lengo: Kufanya matayarisho ya uanzishwaji wa shahada za juu na kupitia mihutasari iliyopo**

Kamati ya uanzishaji wa shahada za juu za idara za mawasiliano ya anga na uhandisi mitambo imeaanza kazi.

Mihutasari ya masomo ya idara za umeme na kompyuta imepitiwa na kurekebishwa**.**

**5.5 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA YA ELIMU AFISI YA PEMBA KATIKA KIPINDI CHA JULAI-SEPTEMBA 2011/2012**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba inatekeleza malengo yake kupitia muundo wa Divisheni kama ifuatavyo:-

**DIVISHENI YA MIPANGO NA SERA**

Katika kipindi cha Julai /Septemba Divisheni hii imekuwa ikisimamia ujenzi wa :-

- Skuli za sekondari za wilaya chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia
- Ujenzi wa kituo cha elimu mbadala Wingwi chini ya ufadhili wa Benki ya Afrika (ADB) na
- Miradi ya uimarishaji wa elimu ya msingi chini ya SMZ.

**DIVISHENI YA UTUMISHI NA UENDESHAJI**

Divisheni pamoja na mambo mengine ina majukumu ya kuwahudumia wafanyakazi wote wa **WEMA** Pemba ambao ni 3759.

Kwa upande wa likizo za watumishi, Wizara (Afisi kuu Pemba) imejitahidi kuweza kuondoa malimbikizo ya madeni ya likizo la miaka miwili ambapo jumla ya shilingi 96,160,000/= zimelipwa kwa kumaliza deni la 2008/2009.Matayarisho ya kulipa likizo kwa mwaka 2010 yameshafanyika na wafanyakazi 210 wanatarajiwa kulipwa.

Aidha, wastafu wote hulipwa fedha mara tu wanapopata barua za kustaafu. Kwa jumla kuanzia Julai/Septemba 2011 wafanyakazi 15 wamestaafu.

Divisheni imeweza kutoa mafunzo kuhusu stadi za maisha ambazo zinajumuisha VVU,UKIMWI na jinsia katika skuli zote , Vyuo vya ualimu –CCK na Benjamin W. Mkapa na kwa walimu wakuu na walimu wa ushauri nasaha.

Kwa upande wa Elimu Mjumuisho, mafunzo kadhaa yameweza kufanyika yakiwemo mafunzo juu ya matumizi ya Braille kwa wanafunzi 24 wasioona na walimu wao,mafunzo ya walimu 65 wa Kangagani na Michenzani juu ya matamshi,ubadilishaji tabia na uchunguzi.Aidha mafunzo juu ya utafiti wa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa skuli 145 za Pemba.

**Changamoto:**

Kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano hakuna ajira iliyofanywa kwa kada za madereva, walinzi, wahudumu, maabara na kompyuta.Aidha tatizo la sehemu hizi linazidi kuongezeka kwa vile wafanyakazi wanastaafu, kuacha kazi au kufariki.

**DIVISHENI YA ELIMU YA SEKONDARI**

Divisheni imeweza kutembelea jumla ya skuli 40 kwa lengo la kuangalia maendeleo ya skuli na utekelezaji wa mipango ya skuli hizo.

**Changamoto:**

- Upungufu wa walimu hususan walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati.Hali ya upungufu ni kama ifuatavyo:Wilaya Chake Chake upungufu 107,Mkoani 127,Wete 106 na Micheweni 62 .
- Uhaba wa vifaa vya Sayansi na Kemikali.
- Skuli nyingi hazina maabara na Maktaba
- Utoro wa wanafunzi.

**DIVISHENI YA ICT**

Divisheni ya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari imeweza kutekeleza yafuatayo:-

- Kutoa mafunzo kwa walimu wakuu na walimu wa takwimu kupitia mradi wa TZ 21.
- Kituo cha walimu cha Michakaeni kimo katika majaribio ya TZ 21 ya Basic Education na kimeanza kufungwa mitambo.

**DIVISHENI YA UPIMAJI NA TATHMINI**

**Yafuatayo yameweza kutekelezwa:-**

- Kufuatilia upatikanaji wa gari na boti kwa ajili ya matayarisho ya usafirishaji wa mitihani ya taifa.
- Kutoa vyeti vya kumalizia masomo ya kidato cha pili .Jumla ya vyeti 62 vilitolewa kwa wahusika.
- Upokeaji wa mapendekezo ya walimu wasimamizi kutoka maskulini.
- Kupanga usimamizi katika mfumo wa vitabu.
- Utoaji wa vitabu vya usimamizi wa mitihani ya kidato cha pili na darasa la saba .
- Upokeaji wa orodha ya watihaniwa wa darasa la saba na kumi kutoka Unguja na kuwakabidhi walimu wakuu.
- Kupanga makisio mbali mbali yahusuyo ufanikishaji wa mitihani ya taifa.
- Kupokea majina ya wasimamizi wenye matatizo na kufanya marekebisho.

**OFISI YA MKAGUZI WA ELIMU –PEMBA**
Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu imefanikiwa kufanya ukaguzi wa aina mbali mbali katika skuli 46 ukiwemo ukaguzi mkuu, ukaguzi wa usajili na maalum.

**Changamoto:**

- Baaadhi ya changamoto ni: Idadi ya wakaguzi bado ni ndogo, hata hivyo mapendekezo yameshafikishwa Wizarani.
- Kwa mujibu wa tathmini ya skuli zilizokaguliwa, skuli nyingi hazina hati miliki.Skuli nyingi hazipo katika maeneo mazuri,baadhi ya skuli zina majengo mabovu,yapo majengo mengi ambayo yanasubiri kuezekwa na kukamilishwa,wingi wa wanafunzi madarasani, utoro mkubwa wa wanafunzi kwa mfano skuli ya Micheweni na upungufu wa walimu katika skuli nyingi.

**5.6 MAONI/MAPENDEKEZO YA KAMATI**

- Kamati haikuridhika na utekelezaji wa malengo ya Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), kutokana na kushindwa kufikia malengo hayo kwa karibu asilimia 70, kuna haja kwa Wizara kukutana na Mhe. Rais ili kujenga hoja juu ya changamoto za msingi zinazokikabili Chuo pamoja na athari zake katika maendeleo ya baadae ya Chuo ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangia kutofikiwa kwa malengo ya Chuo.
- Kamati inaishauri Serikali kutumia zaidi vyuo vyake vikuu vya ndani katika kufanya tafiti, kongamano na semina mbali mbali ili kupunguza gharama za uendeshaji wa tafiti hizo pamoja na kuwapa nafasi zaidi wataalamu wetu.
- Katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la upatikanaji wa fedha kwa wakati kutoka SMZ na BADEA hali ambayo inachangia kuchelewesha kumalizwa ujenzi wa Chuo kama ilivyokusudiwa. Hivyo kuna haja kwa Serikali na washirika wa maendeleo kuzingatia uingizwaji wa fedha kwa muda uliopangwa.
- Kamati imeridhika kuwepo kwa udanganyifu wa aina mbali mbali uliofanyika katika mitihani ya kidato cha nne ya mwaka 2011na kupelekea Baraza la Mitihani la Tanzania NECTA kufuta matokeo ya wanafunzi wote waliothibitishwa kufanya udanganyifu huo.Hata hivyo kamati imelishauri Baraza la Mitihani kupitia upya adhabu iliyotolewa ya miaka mitatu ya kutorejea kufanya mitihani hiyo kwa kuzingatia athari ya muda huo kwa vijana.
- Pia kwa upande mwengine, Kamati imeona kuwa hivi sasa kumejitokeza hali ya utatanishi baada ya Kamati kukutana na Kamati ya wazee ya wanafunzi ambao wameathirika na kufutiwa matokeo ya mitihani hiyo.Hivyo Kamati inaishauri Serikali kutokana na hali iliyojitokeza kufanya uchunguzi wa kina juu ya suala hilo kwani wazee walio wengi hawakuridhika na maamuzi yaliyotolewa .
- Aidha, Kamati imelishauri Baraza la Mitihani Tanzania kuanzisha ofisi yake Zanzibar kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi za usimamizi wa mitihani katika sehemu ya pili ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kukamilisha uchunguzi juu ya kuwepo kwa tuhuma za baadhi ya wasimamizi (walimu) wa mitihani ya kidato cha nne ya mwaka 2011 kushiriki katika udanganyifu wa mitihani hiyo, ili wizara iweze kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa wahusika wote watakaobainika kushiriki katika udanganyifu huo.
- Kwa kuwa pia kuna tuhuma za maafisa wa taasisi nyengine kushiriki katika udanganyifu wa mitihani hiyo ,kuna haja kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani Tanzania kufanya uchunguzi zaidi ili kuisaidia Serikali kubaini wahalifu hao na kuchukuliwa hatua za kisheria.
- Kamati imeishauri Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kuendelea kuelimisha vyuo vikuu mbali mbali nchini kikiwemo SUZA, faida na madhara ya kuanzishwa Mfumo wa pamoja wa udahili (CAS) wa wanafunzi wa vyuo hivyo.
- Wizara , kupitia Mradi wa uimarishaji huduma za maktaba ,iangalie njia mbadala zinazokwenda sambamba na wakati uliopo katika kuimarisha mfumo wa utoaji wa vitabu vya marejeo (references) kupitia njia za mitandao ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo
- Kamati imebaini kuwa Skuli nyingi za zamani hazina sehemu ama vyumba kwa ajili ya matumizi ya maktaba hivyo kuna haja kwa wizara kuanzisha utaratibu huo.

- Kamati imeridhika na maendeleo ya mradi wa ujenzi wa baadhi ya skuli za sekondari ikiwemo Skuli ya Dole ambapo imeishauri Wizara kuzingatia umuhimu wa uwekaji uzio, mabweni ya wanafunzi pamoja na nyumba za walimu.
- Kamati imeishauri Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kutafuta njia muafaka za kukabiliana na changamoto ya urejeshwaji wa madeni ya zamani pamoja na namna ya ulipaji wa mikopo kwa watu binafsi.Bodi kwa kutumia sheria ya mikopo ya elimu ya juu iliyopo ina jukumu la kuhakikisha kuwa kasoro hizo zinaondoka.
- Kamati inaipongeza Skuli ya Mtopepo kwa mafanikio yaliyopatikana na kuwa ni skuli iliyotoa mfano katika kujenga nidhamu ya ufanyaji wa mitihani pamoja na matokeo kwa kidato cha pili na nne kwa mwaka 2011.
- Ipo haja kwa Serikali kuwa na kiwanda chake cha uchapishaji mitihani ili kuepuka kuendelea kutumia gharama nyingi za nje za uchapishaji pamoja na kuondoa wasi wasi wa uvujaji wa mitihani na kupelekea udanganyifu.
- Kamati inapendekeza kupitiwa malipo ya wahadhiri wa vyuo vikuu vya Zanzibar ili yaendane na hadhi yao, kwani malipo yaliyopo hayaendani na elimu waliyonayo katika soko la ajira.
- Kamati imebaini kuwa miradi mingi ya ujenzi wa Skuli Pemba (Mfano Skuli ya Sekondari Wilaya-Mauwani Kiwani) haikuzingatia ujenzi wa dahalia za wanafunzi, hivyo imeishauri Serikali kuzingatia hali hiyo hasa kwa skuli ambazo zipo mbali na makaazi ya wanafunzi.
- Kamati imeipongeza Wizara kwa hatua nzuri iliyofikiwa ya Mradi wa ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa.Hata hivyo imeishauri Serikali kuanzisha Skuli ya mazoezi (maandalizi na msingi) ndani ya Chuo ili kurahisisha upatikanaji wa mafunzo ya vitendo kwa walimu.
- Kamati imebaini kuwa sehemu iliyotengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa maktaba Pemba ni ndogo, hasa kwa malengo ya mahitaji yaliyopo na baadae.Wizara katika kukabiliana na changamoto hiyo, kuna haja ya kuhakikisha kuwa wanalitumia vyema eneo hilo ili kufikia malengo na kukidhi mahitaji ya watumiaji.
- Kuhusu vipaumbele vya utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kuwa licha ya kuweka vipaumbele vyake katika kuwapatia mikopo zaidi wanafunzi katika kada ya Sayansi, kuna umuhimu pia wa kuzingatia hali ya usawa katika kufaidika na rasilimali za nchi zilizopo.Hivyo ipo haja kwa serikali kutenga asilimia maalum ya mikopo hiyo kwa wanafunzi wa kada ya sanaa (Arts) na nyenginezo kwa lengo la kuleta usawa katika kufaidika na rasilimali zilizopo.

## 5.7 MAAGIZO YA KAMATI

- Licha ya kuwepo kwa hali isiyoridhisha na ucheleweshwaji wa ujenzi unaoendelea wa mradi wa Skuli 3 za Sekondari za PAJE MTULE,TUNGUU NA DIMANI ,Wizara ihakikishe kuwa ujenzi wa skuli hizo unaoendeshwa na Kampuni ya ELECTRIC INTERNATIONAL Co. Ltd ya Dar Es Salam, unakuwa na viwango vilivyokusudiwa na unazingatia wakati kwa kwa mujibu wa makubaliano ya kisheria yaliyopo.
- Kamati inaiagiza Wizara kutumia busara ili mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao sasa ni waajiriwa katika taasisi za Serikali iweze kurejeshwa .Deni la shilingi bilioni 8 kwa waliokopa ni kubwa na linaathiri maendeleo ya Bodi.
- Kamati inaiagiza Wizara katika bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 kuhakikisha kuwa inaainisha ada ya shilingi milioni mia 3 ya watahiniwa wa kidato cha nne kwa lengo la kurahisisha ulipaji wa ada hizo kwa wakati.
- Kwa kuwa Jengo linaloendelea kutumiwa na Afisi za Bodi ya Upimaji na Tathmini imetolewa taarifa na Mamlaka ya Mji Mkongwe kuwa halifai kwa ajili ya matumizi ya ofisi kutokana na hali mbaya ya ubovu kwa zaidi ya miaka 10, kamati inaagiza afisi za Bodi zihamishwe na kutafutiwa sehemu nyengine ili kulinda usalama wa wafanyakazi.
- Kamati imeitaka Wizara ya Elimu kufuatilia kwa karibu matatizo yanayoikabili Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Kengeja yakiwemo (hali ya mfumo wa maji machafu ,upungufu wa walimu wa ufundi katika idara ya umeme,uhaba wa mabweni pamoja na huduma za afya) .

## 5.8 HITIMISHO

Kwa ujumla Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutathmini changamoto za msingi zinazokikabili Chuo Kikuu cha Taifa cha SUZA ili kuweza kukijengea mustakbali mzuri wa maendeleo Chuo hicho.Aidha kuhusu ajira za walimu ambazo zimekwama katika Wizara ya Nchi,Ofisi ya Rais,Utumishi wa Umma na Utawala Bora kamati inaisisitiza wizara ya elimu kushirikiana na wizara hiyo ili kuhakikisha kuwa ajira hizo zinafanyika kwa mujibu wa utaratibu na mahitaji yaliyopo.

## 6.0 WIZARA YA USTAWI WA JAMII MAENDELEO YA WANAWAKE, VIJANA NA WATOTO

Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imeanzishwa kwa lengo la kuinua na kuimarisha hali za Wanawake, Watoto, Vijana na Watu walio katika makundi maalum ya Wazee wasiojiweza, Mayatima na wanaoishi katika mazingira magumu zaidi.

Aidha Wizara inafanyakazi kupitia Idara 5 na Ofisi kuu Pemba. Idara hizo ni; Idara ya Mipango, Sera na utafiti, Idara

ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Maendeleo ya Vijana, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Idara ya Ustawi wa Jamii na Ofisi kuu Pemba.

### 6.1 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA MWAKA ULIOTANGULIA 2010/2012

- **Wizara ihakikishe kuwa inasimamia ipasavyo maelezo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya kuongezwa bajeti ya Wizara hiyo ambayo iliyopo inaonekana haikidhi haja katika Wizara muhimu ya Ustawi wa Jamii.**

Wizara imo katika mchakato wa kufanya tathmini ya uwezo wa Wizara Kifedha, Rasilimali watu na vifaa. Matokeo ya tathmini hiyo yataonesha kwa kiasi gani wizara inaathirika kwa bajeti ndogo na hivyo kujenga hoja Serikalini ya kuongezwa kwa bajeti ya Wizara.

- **Wizara ihakikishe inakipatia Kituo cha Kulelea Watoto Mazizini jenereta la dharura kwa ajili ya huduma ya umeme ili kuepuka matumizi mabaya ya vibatari hali inayoweza kuchafua mazingira mazuri ya usafi wa jengo hilo.**

Wizara imechukua juhudi ya kununua Jenereta dogo ili kukidhi mahitaji ya dharura. Aidha mipango iko mbioni ya kununuliwa jenereta jengine kubwa litakalotosheleza mahitaji.

- **Kamati imeitaka Wizara iandae taarifa maalum za database za maendeleo ya kila mtoto anaelelewa katika kituo cha Mazizini ili kuelewa kumbukumbu zake kwa ajili ya maendeleo yake ya baadae**

Kwa hivi sasa taarifa za watoto wanaolelewa katika nyumba ya watoto Mazizini zinahifadhiwa katika mfumo wa kukusanya na kuhifadhi taarifa (Database) za Wizara kwa watoto wanaoishi katika Mazingira magumu zaidi. Utaratibu utaandaliwa wa kutayarisha Mfumo wa kukusanya na kuhifadhi taarifa kwa ajili ya watoto wanaoishi katika Nyumba ya kulelea watoto Mazizini pekee.

- **Kamati inaitaka Wizara kumpatia usafiri wa uhakika Mhudumu wa kituo cha Wazee Sebleni.**

Vespa moja imenunuliwa kwa ajili ya kusaidia shughuli za ufuatiliaji katika Makao ya wazee Sebleni.

- **Wizara iharakishe kufungua kituo cha One Stop Center Pemba ili kiweze kuwasaidia wananchi katika kupambana na kesi za udhalilishaji watoto**

Wizara tayari imepatiwa eneo kwa ajili ya kuanzisha kituo hicho katika hospitali ya Chake Chake

### 6.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI

### MUHTASARI WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA FEDHA ZA WAHISANI JULAI – DISEMBA, 2011

| IDARA | JINA LA MRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA KWA MWAKA 2011-2012 | FEDHA ZILIZOTENGWA JULAI-DISEMBA | FEDHA ILIYOTUMIKA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| WANAWAKE NA WATOTO | UHAI,HIFADHI NA MAENDELEO YA MAMA NA MTOTO | 92,165,000 | 77,600,000 | 37,170,000 | 48 |
| MAENDELEO YA VIJANA | UHAI,HIFADHI NA MAENDELEO YA MAMA NA MTOTO | 89,269,500 | 23,217,000 | 19,200,000 | 83 |
| USTAWI WA JAMII | WATOTO WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU | 354,039,000 | 14,789,600 | 14,789,000 | 100 |
| | UHIFADHI WA HAKI ZA | - | 27,726,000 | 27,726,000 | 100 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **MTOTO** | | | | |
| **MIPANGO SERA NA UTAFITI** | **MRADI WA KUIMARISHA JINSIA ZANZIBAR** | - | 146,387,000 | 131,601,500 | 90 |
| **JUMLA** | | **535,473,500** | **289,719,600** | **230,486,500** | 80 |

**6.3 UTEKELEZAJI WA MATUMIZI YA FEDHA**

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,540,000,000/=. Katika kipindi cha mwezi wa Julai hadi Disemba, 2011, Wizara imeingiziwa jumla ya Shilingi Milioni mia sita thelthini na tisa, mia moja na themanini na tatu Elfu, mia tisa na tisini na tisa (639,183,999/=) kwa kazi za kawaida (Recurrent) na Shilingi Milioni mia mbili na thelathini, mia nne na themanini na sita elfu na mia tano (230,486,500/=) kwa kazi za maendeleo (Development).

**6.4 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA YA USTAWI WA JAMII NA MAENDELEO YA VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO**

Wizara kwa kipindi cha miezi sita Julai- Disemba 2011 imetekeleza malengo yake iliyojiwekea kama ifuatavyo;

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

**Lengo: Kuhakikisha kuwa Mapungufu katika Sheria na Sera zinazohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee yanafanyiwa kazi.**

Wizara imefanya kikao na Wataalamu kujadili rasimu ya Sera ya Jinsia Zanzibar, Sera ambayo itakuwa dira katika kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa katika Sera za kitaifa na Kisekta, Mipango, Bajeti na Programu. Kikao hicho kilitoa muongozo wa kurekebisha baadhi ya vipengele vya Sera hiyo na marekebisho hayo tayari yameshaingizwa katika sera hiyo na kukamilika. Sera hivi sasa ipo katika hatua ya kutafsiriwa ili ipelekwe katika vyombo vya maamuzi. Wizara pia imefanya tafsiri ya Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka minne 2011- 2015 kwa lugha ya Kiswahili na imefanikiwa kuchapisha nakala 500 za Mpango Mkakati huo za lugha ya Kiingereza. Nakala hizo tayari zimeshaanza kusambazwa kwa Wadau.

Wizara imo katika hatua ya kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005 ili iende na wakati. Wizara imeandaa jumla ya vikao vitano vya wataalamu kwa kushirikiana na Mtaalamu muelekezi vya kufanya mapitio ya Sera hiyo. Wizara imepokea mapendekezo na kuyaingiza katika Sera hiyo. Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana pia imewasilishwa katika Kongamano la Maadhimisho ya siku ya Vijana na kujadiliwa.

Rasimu ya mwanzo ya Sera ya Hifadhi ya Jamii imetayarishwa na kupitiwa na wataalamu wa ndani wa Wizara pamoja na Kamati nyengine za kisekta kwa kuimarishwa. Aidha vikao vinne vikiwemo vya Kamati Tendaji na Kamati ya Usimamizi (Steering Committee) vilifanyika kujadili uwezekano wa kuwa na Sera moja itayozingatia masuala ya Hifadhi ya Jamii na Ustawi wa Jamii, pamoja na kupendekeza maeneo mengine yanayoweza kuingizwa ili kuimarisha rasimu ya Sera hiyo. Ripoti ya tathmini ya kuingizwa kwenye Sera na muundo wa utaratibu mzima wa kutayarisha Sera uko tayari, na wataalamu wataanza kazi rasmi Machi mwaka huu.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria ipo katika hatua ya kurekebisha Sheria ya Mahkama ya Kadhi ya mwaka 1985. Mapitio ya Sheria hii yamefanyika kufuatia uchambuzi wa sheria zinazowadhalilisha wanawake. Sheria ya Mahkama ya Kadhi ni miongoni mwa sheria zilizobainika kuwa na mapungufu makubwa katika maeneo ya talaka, mgawanyo wa mali wakati wa kuachana na matunzo ya watoto. Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Mahkama ya Kadhi kuangalia mifumo ya Mahakama za Kadhi za nchi nyengine na kukusanya maoni ya wadau mbali mbali (Viongozi wa dini na wanasheria). Jumla ya vikao vinne vya Kamati ya usimamizi na mikutano saba ya wadau ya kukusanya maoni imefanyika na ripoti ya hatua ya mwanzo imewasilishwa kwa wahusika. Hivi sasa, Wizara kwa kushirikiana na Mtaalamu Muelekezi inaandaa Mswada wa Sheria ya Mahkama ya Kadhi.

**Lengo: Kukuza uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

Wizara kupitia watendaji wake imefanya safari mbali mbali za Kikazi kwa Watendaji wake ikiwemo kufuatilia shughuli za Wizara Tanzania Bara na Pemba, kuhudhuria vikao vya Afrika Mashariki Arusha na Dar es Salaam, kuhudhuria katika Uwashaji na Kilele cha Mbio za Mwenge. Aidha, Mheshimiwa Waziri pamoja na Viongozi wa Serikali walihudhuria safari ya kujifunza nchini China.

Wizara ilihudhuria katika mkutano wa nchi za Maziwa Makuu nchini Uganda na Arusha uliozungumzia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia.

Wizara pia imefanikiwa kuandaa na kuchapisha Mpango wa utekelezaji wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein. Wizara pia imefanikiwa kuandaa taarifa za awali za Mipango ya matumizi ya muda wa kati (MTEF) ya Wizara kwa kuziwasilisha Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya kutayarisha 'ceiling' ya Wizara.

Wizara imetayarisha maandiko ya miradi mbali mbali ya Wizara. Andiko la mradi la uchambuzi wa takwimu kijinsia lilitayarishwa, na tayari limeshapatiwa mfadhili na mradi utaanza kazi wakati wowote kuanzia mwezi wa Machi.

Aidha Wizara ilifanikiwa kutayarisha maandiko ya miradi minane kwa kuzingatia utekelezaji wa MKUZA II na kuyawasilisha Ofisi ya Rais, fedha, uchumi na Mipango ya Maendeleo. Wizara aidha iliandaa andiko la kufanya utafiti wa udhalilishaji wa kijinsia kwa Wilaya zote Unguja na Pemba ili kuelewa ukubwa wa tatizo hili. Andiko hili linatarajiwa kuwasilishwa katika Kikao cha Kamati ya Baraza la Mapinduzi kwa kujadiliwa.

Wizara imefanya warsha ya siku tatu kwa Watendaji wake kuibua ajenda za utafiti na kutoa mafunzo ya jinsi ya kutayarisha maandiko ya miradi. Jumla ya ajenda 9 za utafiti zimeibuliwa kwa Wizara.

**Lengo: Kuimarisha uratibu wa muitiko wa wadau na watoa huduma wa masuala yanayohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.**

Wizara imeandaa Muongozo wa watoa huduma kwa waathirika wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Muongozo umeandaliwa na Wataalamu waelekezi kwa kushirikiana na kamati ya Wataalamu kutoka katika sekta za Afya, Polisi, Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ZAFELA na Kamati za kuzuia vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia za Mikoa na Shehia.

**Lengo: Kuimarisha ukusanyaji wa taarifa, uwekaji wa kumbukumbu na kutayarisha mfumo wa mawasiliano wa Wizara.**

Wizara imeandaa Mpango wa ufuatiliaji na tahmini kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Wizara na tayari unatumika kukusanya taarifa za utendaji wa Wizara za kila mwezi. Fomu za ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara zimetayarishwa na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Fomu hizo zimezingatia mifumo ya ripoti zote zinazotakiwa kuripotiwa na Wizara kama vile taarifa za Ilani ya Uchaguzi, Ripoti ya Bango tita, Ripoti za Ofisi ya Rais, fedha, Uchumi na mipango ya maendeleo n.k.

Wizara pia imefanya mapitio ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa masuala ya jinsia kwa kuingiza viashiria vya MKUZA pamoja na Mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW). Mfumo ulijadiliwa na wadau, pamoja na kufanyiwa majaribio ya kutumika kwake (Pre testing).

Wizara ina mkakati wa kukiimarisha kitengo cha habari. Pendekezo la Mradi wa Uimarishaji wa kitengo hicho lipo tayari na limo katika hatua ya kutafutiwa fedha ili kukiimarisha kitengo hicho kiweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Wizara aidha, imefanikiwa kutayarisha vipindi 22 na kuvirusha katika redio na televisheni, imeandaa makala 20 zinazohusu walengwa wa Wizara na kuyatoa katika gazeti la Zanzibar Leo, na imetayarisha habari 69 za matukio mbali mbali ya Wizara na kuzirusha katika Redio na Televisheni.

## IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

**Lengo: Kukuza uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

Wizara kwa kushirikiana na mtaalamu mwelekezi imeanza taratibu za kufanya tathmini ya uwezo wa wizara ili kujua mapungufu yaliopo katika raslimali watu, raslimali fedha na hali ya kiutendaji. Wizara imeunda kamati ya kitaalamu inayoshirikiana na mtaalamu mwelekezi. Hadi kufikia Disemba 2012, hadidu rejea na taarifa ya awali ya namna ya utekelezaji wa zoezi hilo (inception report) vilikua vimekamilika. Zoezi la tathmini linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2012. Wizara imetayarisha mpango wa manunuzi na daftari la kudumu la mali za serikali (fixed asset register) kwa mujibu wa Sheria ya manunuzi ya mwaka 2005.

Wizara imenunua vifaa vya ofisi ili kuwezesha utekelezaji wa kazi za kila siku. Vifaa vilivyonunuliwa kwa kipindi hichi vinajumuisha: vifaa vya usafi na vya kuandikia, magazeti, kalenda, vipando 2(vespa) na mafuta. Wizara pia imefanya matengenezo ya gari na vifaa vya ofisini pamoja na kufanya matengenezo madogo ya majengo ya ofisi na

kugharamia matumizi ya umeme na maji.

Wizara imetoa huduma kadhaa kwa wafanyakazi ili kuwapa uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Huduma zilizotolewa ni kama zifuatazo:

- Wafanyakazi 18 wakiwamo walinzi, madereva na wahudumu wa nyumba za wazee wameshonewa nguo/sare za kazi.
- Wafanyakazi 18 waliokwenda likizo wamelipwa posho ya likizo, aidha wafanyakazi 23 (madereva 7 na walinzi 16) wamelipwa posho la malipo ya baada ya saa za kazi.
- Jumla ya wafanyakazi 5 wamesaidiwa malipo ya ada ya masomo ya elimu ya juu katika vyuo wanavyojiendeleza. Wafanyakazi hao wanasoma katika vyuo vikuu vya Tanzania na Uganda.

Wizara imeweza kuunda kamati mbali mbali ili kuimarisha uwajibikaji wa pamoja (collective responsibility). Kamati hizo ni Kamati Tendaji, Kamati ya Uongozi na Bodi ya Zabuni.

Wizara pia imeanzisha utaratibu wa kufanya vikao kwa siku ya Jumatatu ya kila wiki kwa watendaji wakuu wa Idara zote kukutana na kupeana taarifa za utekelezaji wa Idara zao, na kuimarisha mawasiliano juu ya utendaji wa kazi za Wizara. Vikao hivi vinaendeshwa chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu.

**IDARA YA USTAWI WA JAMII**

**LENGO: Kuimarisha uratibu wa muitiko wa wadau na watoa huduma kwa masuala yanayohusu wanawake, vijana, watoto na wazee**

Kuendelea kutoa misaada ya kijamii kwa wasiojiweza ambapo jumla ya familia 52 zilisaidiwa Tsh. 15,000/- kwa kila familia na watoto 47 walisaidiwa Tsh 7,000/- kila mmoja kwa kila mwezi.

Aidha jumla ya akina mama 6 waliojifungua pacha tatu walipatiwa msaada wa maziwa Unguja na Pemba.

Wizara iliendelea kulipa fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali wakiwa kazini, ambapo jumla ya wafanyakazi saba walilipwa fedha katika kipindi hicho na wanne kati yao walimaliziwa deni lao. Aidha, Wizara imeandaa Waraka wa kuhamishia shughuli zote za Fidia kwenda Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi kiuchumi na Ushirika. Hadi sasa kiasi chote cha fidia kinachodaiwa ni Tsh 30, 555,326.51/- kwa Unguja na Tsh 55,730,849/- kwa Pemba.

Wizara imeendelea kutoa matunzo na huduma kwa wazee wanaoishi katika makaazi ya wazee. Katika Makaazi ya wazee Welezo Wizara iliupatia Uongozi wa Makaazi hayo jumla ya Tsh. 3, 000,000 kila mwezi kama ni mchango wa Serikali katika kugharamia uendeshaji wa Makaazi hayo. Aidha, Wizara imefanikiwa kuongeza posho la wazee kutoka Tsh. 25,000/- hadi 40,000/- kwa mwezi kwa wazee wa Sebleni na Tsh. 7,000/- hadi 15,000/- kwa mwezi kwa wazee wa makaazi ya wazee Welezo. Ongezeko hilo lilianza mwezi wa Oktoba 2011. Vile vile, Idara imenunua Vespa moja kwa ajili ya kusaidia shughuli za ufuatiliaji katika Makaazi ya Wazee Sebleni.

Wizara vile vile ilizika jumla ya maiti kumi na nne (14) zisizokuwa na wenyewe, na jumla ya shs.1, 631,000/- zilitumika katika shughuli hiyo. Wizara imepokea jumla ya Shs. 65,714,000/- kwa ajili ya ukarabati wa jengo lililoungua moto katika makaazi ya Wazee Sebleni. Kati ya fedha hizo jumla ya shs. 31,714,000/- zimetumika katika kazi hiyo, na ukarabati bado unaendelea.

Sherehe ya Siku ya wazee Duniani ilifanyika tarehe 01.10.2011 katika Makaazi ya Wazee Sebleni. Ujumbe wa Siku ya wazee mwaka 2011 ni "Kuongezeka kwa changamoto na fursa kwa wazee duniani".

Wizara kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia watoto UNICEF, ilifanya Uzinduzi wa Miongozo ya Kitaifa ya Uhifadhi na Ustawi wa Watoto Zanzibar.

Wizara kwa kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto kwa kushirikiana na wadau wake wa Maendeleo UNICE, imetoa mafunzo ya siku 4 kwa wataalamu sita watakaotumika kufundisha wadau mbali mbali Miongozo ya Kitaifa ya Uhifadhi na Ustawi wa Watoto Zanzibar. Vile vile, Wizara imetoa mafunzo ya Miongozo hiyo kwa kamati ya kitaifa pamoja na kamati zote za Hifadhi ya Mtoto za Wilaya Unguja na Pemba.

Wizara ilifanikiwa kuwalipa wafanyakazi wawili posho la kujikimu kwa safari za nje ya nchi kikazi. Fedha hizi zililipwa ikiwa ni deni la nyuma tokea Idara ya Ustawi wa Jamii ipo chini ya Wizara ya Afya.

**LENGO**: **Kuangalia hali halisi ya haki na maendeleo ya Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee zinafuatiliwa na**

**kutolewa taarifa kwa wakati**

Wizara katika kuimarisha huduma kwa watoto wanaolelewa katika kituo cha kulelea watoto Mazizini, imeupatia uongozi wa kituo hicho Shs. 3, 000,000/- kwa ajili ya gharama za uendeshaji kila mwezi. Aidha, Idara iliwapatia watoto wote 47 wanaolelewa kituoni hapo pesa za mfukoni Shs. 7,000/- kila mtoto kwa kila mwezi, pamoja na nguo za sikukuu.

Wizara pia imefanya utanuzi wa jiko la nje katika Nyumba ya Watoto Mazizini, pamoja na kuliwekea zege eneo la nyuma ya nyumba hiyo. Sambamba na hilo, Wizara ililipia gharama za upakuzi na usafirishaji wa kontena la vifaa vya watoto wanaolelewa katika Nyumba ya Kulelea watoto Mazizini ambalo ni msaada kutoka kwa Bi. Mala wa Omani. Wizara katika kuunga mkono jitihada za wadau iliupatia uongozi wa Kituo cha Kulelea Watoto cha S.O.S jumla ya Tsh. 1, 000,000/- kama ni msaada wa kusaidia gharama za uendeshaji wa kituo hicho.

Wizara katika kuratibu shughuli za uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto vya watu binafsi, ilifanya ukaguzi wa vituo vinavyomilikiwa na watu binafsi ili kuwapatia miongozo ya utoaji wa huduma na uendeshaji wa vituo hivyo. Jumla ya vituo vitano vilitembelewa, kufanyiwa ukaguzi na kupatiwa miongozo.

Wizara kwa kupitia Kitengo cha Hifadhi ya mtoto, ilifanya mikutano mitano ya Kamati za Kitaifa za Ulinzi na Hifadhi ya Mtoto Unguja na Pemba.

Aidha Wizara imeweza kuendesha zoezi la dharura la kuwatambua wanawake na watoto walioathirika katika ajali ya MV Spice Islanders. Zoezi limefanyika kwa kanda ya Unguja na rasimu ya ripoti ya mwisho imeshapelekwa katika ofisi husika.

Wizara katika kusimamia taarifa za watoto wanaoishi katika mazingira magumu, ilifanya mkutano wa siku mbili wa kuupitia mfumo wa kutunza taarifa za Watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, pamoja na wadau wanaoshughulikia masuala ya watoto. Mkutano huo ulijadili changamoto zinazowakabili watumiaji wa mfumo wa kutunzia taarifa na namna ya kuuboresha mfumo huo.

Idara pia ilifanya mkutano na wadau kujadili maendeleo ya shughuli za Watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi hapa Zanzibar.

## IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA

**LENGO: Kukuza uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

Wizara kwa kushirikiana na Mtaalamu mwelekezi ilifanya zoezi la kuangalia hali halisi ya vijana kijamii, kiuchumi na kisiasa. Vikao vitatu, kimoja cha Idara na Mshauri Mwelekezi na viwili vya Kamati ya Wataalamu vilifanyika. Rasimu ya tathmini ya hali halisi ya Vijana Zanzibar imeandaliwa. Wizara pia ilifanya vikao sita vya ndani kwa wafanyakazi wake kutathmini utekelezaji wa majukumu ya Idara.

Wizara pia, ilihudhuria Mikutano ya Vijana ya Jumuiya za Madola. Maafisa wawili walihudhuria Kongamano la Vijana Nchini Misri. Kongamano hilo lilikuwa na lengo la kuwakutanisha vijana wa nchi za ukanda wa Mto Nile kuzungumzia mustakbali wa maendeleo ya vijana wa nchi hizo.

**LENGO: Kuhamasisha uimarishaji hali za kiuchumi, utamaduni na maendeleo kwa wanawake, vijana, watoto na wazee**

Wizara ipo katika hatua za mwisho za uandaaji wa Baraza la Vijana**.** Idara imefanya vikao vitatu vya kuingiza maoni ya Wadau katika Rasimu ya Baraza la Vijana. Rasimu ya Katiba ya Baraza la Vijana na Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana zimewasilishwa katika Kongamano la kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani ili kupata maoni ya Vijana. Rasimu ya Baraza la Vijana ilifanyiwa marekebisho kutoka kwa Wadau wa Maendeleo ya Vijana. Kwa hatua hii Rasimu ya Katiba ya Baraza la Vijana imepelekwa katika kikao cha Makatibu Wakuu kwa kujadiliwa.

Wizara inaendelea na uratibu wa kufuatilia utekelezaji wa Mfuko wa Norway kupitia UN Habitat. Idara ilisimamia zoezi la kuvitangaza vikundi vilivyoshinda katika kupata Ruzuku ya Mfuko wa Norway. Vikundi 6 (Unguja 2 na Pemba 4) vimefanikiwa kupata fedha kupitia UN Habitat. Wizara imeviwezesha vikundi sita (6) vya vijana viwili (2) kutoka Unguja na Vinne (4) kutoka Pemba kupata msaada wa Mfuko wa NORWAY wenye thamani ya dola za kimarekani laki moja **(US$100,000)** unaoendeshwa na kusimamiwa na Shirika la UN HABITAT. Kwa hatua ya mwanzo tayari vikundi hivyo 6 wameshapewa asilimia sitini ya fedha hizo na asilimia arubaini watapatiwa mara tu watakaporejesha mahesabu ya matumizi ya fedha za awali.

Aidha, Wizara imesimamia upatikanaji wa fedha kwa vikundi vyote vilivyobahatika kupata Ruzuku ya fedha za Mfuko wa Vijana kutoka Serikali ya Norway. Vikundi 6 vilivyochaguliwa na 3 ambavyo havikuchaguliwa vilipatiwa mafunzo ya kuendesha miradi na kuandika ripoti ya fedha.

Wizara katika kuwahamasisha Vijana kujitafutia ajira imefanikiwa kuwahamasisha vijana 700 kuunda Jumuiya ya kutunza usafi wa Mji wa Zanzibar. Vijana 135 wamepatiwa ajira za muda, kati yao 45 wamepatiwa ajira ya usafi wa Mji na vifaa vya kufanyia usafi vyenye thamani ya sh. 8,500,000/= zilizotolewa na wahisani wa ndani. Vijana 90 wamepatiwa ajira katika shirika la simu la Zantel na Vijana 5 wamepata ajira ya kudumu Zantel.

Wizara pia imefanikiwa kuanzisha Kilimo cha majaribio cha Maua ya Rosela na Mbogamboga kwa Vijana. Wizara ilifanya utaratibu wa kuwapatia Vijana eneo Tunguu la kilimo cha Maua ya Rosela na Mbogamboga. Mtaalamu wa kusaidia katika kilimo cha Maua na mboga mboga amepatikana. Upatikanaji wa Miundo mbinu ya Maji pamoja na ununuzi wa vifaa na Mbegu kwa ajili ya shamba hilo umefanyika kwa msaada wa Wizara.

**LENGO: Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.**

Wizara ilishiriki katika Maandalizi na kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2011 Mkoani Dar es Salaam na Mara. Idara aidha ilifanya safari mbali mbali za kikazi Tanzania bara na Pemba. Jumla ya Miradi 33 yenye thamani ya sh. Bilioni 1,897,166,431/= imezinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi Unguja na Pemba.

Ziara ya mafunzo ya kuangalia shughuli za maendeleo ya mikopo kwa SACCOS za Dar es Salaam zinazopatiwa huduma za kifedha na Benki ya CRDB imefanyika. Vikao kati ya Uongozi wa Wizara na Benki ya CRDB vya kuandaa Mpango wa Mikopo kwa Vijana vilifanyika.

## IDARA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO

Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ni Idara yenye jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Haki za Wanawake na Watoto pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mikataba ya Kimataifa inayohusu Wanawake na Watoto.

**Lengo: Kuhakikisha kuwa mapungufu katika Sheria na Sera zinazohusu Wanawake na Watoto zinafanyiwa kazi.**

Wizara katika utekelezaji wa lengo hilo, ilizindua rasmi matokeo ya utafiti juu ya udhalilishaji wa watoto Siku ya tarehe 22 Septemba 2011. Uzinduzi huo ulifanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Bwawani ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi. Uzinduzi huo ulifuatiwa na semina ya waandishi wa habari kutoka katika baadhi ya vyombo vya habari Tanzania pamoja na maandamano ya watoto na michezo ya kuigiza. Aidha, taasisi mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya watoto zilijikubalisha kuchukua dhamana ya kuondoa udhalilishaji wa watoto Nchini. Taasisi hizo ni pamoja na; Sekta ya Afya, Sekta ya Polisi, Sekta ya Elimu pamoja na taasisi za kijamii.

Wizara pia imeandaa na kuwasilisha rasimu ya mwisho ya taarifa ya utekelezaji wa mkataba wa Haki za mtoto (CRC). Taarifa hiyo imeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau wanaoshughulikia masuala ya watoto. Aidha Idara imeiwasilisha taarifa hiyo Tanzania Bara kwa lengo la kuiunganisha pamoja na kuwa Taarifa moja ya Tanzania. Taarifa hiyo imeshawasilishwa Nchini Geneva kwa hatua zinazofaa.

Pamoja na hayo, Idara iliandaa warsha ya siku mbili iliyofanyika katika Hoteli ya Mazson iliyohusu uandaaji wa rasimu ya awali ya mpango wa utekelezaji wa sheria ya mtoto kwa kuzingatia uzoefu wa mpango kama huo kutoka Tanzania Bara. Aidha Idara iliandaa warsha ya wadau wa utekelezaji wa shughuli za watoto kwa lengo la kuijadili rasimu hiyo.

**Lengo: Kuhamasisha uimarishaji wa hali za kiuchumi, utamaduni na maendeleo kwa wanawake na watoto**

Katika kuhakikisha kuwa hali za kiuchumi, utamaduni na maendeleo ya wanawake zinaimarishwa, Idara iliwawezesha jumla ya wajasiriamali sita kushiriki katika maonesho ya wajasiriamali ya Nchi za Afrika Mashariki yaliyofanyika Kigali Rwanda kuanzia tarehe 5/8 hadi tarehe 6/8/2011. Aidha Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko iliwawezesha wajasiriamali wa Zanzibar kushiriki katika maonesho ya 35 ya Saba Saba huko Dar-es-Salaam. Jumla ya vikundi 54(42 kutoka Unguja na 12 kutoka Pemba) vilishiriki maonesho hayo. Unguja wanawake 36 na wanaume 6 na Pemba wanawake 10 na wanaume 2.

Wizara pia, ilifanya ziara ya kuvitembelea vikundi mbalimbali vya wanawake viliopo Bweleo kwa ajili ya kutathmini maendeleo na mahitaji yao. Jumla ya Vikundi vinane (8) vilitembelewa. Vikundi hivyo ni pamoja na Bado Tupo, Imara Group, Tusife moyo, Chetu cha Bweleo, Ushirika wa lengo moja, Hiari ya Moyo, Mmewezaje na Ukweli ni njia

Safi. Hata hivyo ilionekana kuwa vikundi hivyo vinahitaji mafunzo ya Ujasiriamali ili kuleta ufanisi katika kazi zao.

Katika kuratibu shughuli za uanzishaji wa Benki ya Wanawake, Idara ilifanya ziara katika taasisi za kifedha pamoja na SACCOS ili kupata maoni ya kuendesha taratibu za uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Taasisi zilizotembelewa ni pamoja na CRDB, WEDTF, Mfuko wa Kujitegemea, Changamoto, PRIDE na Konde SACCOS. Aidha tayari Idara imefanya mawasiliano na Wizara ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya kupatiwa jengo la iliyokuwa Benki ya Watu wa Zanzibar liliopo Mwanakwerekwe. Pamoja na hayo ilionekana kuwa kuanzisha Benki ni gharama na itawafaidisha zaidi wanawake wenye uwezo kuliko wasio na uwezo kutokana na vigezo vilivyowekwa na Benki Kuu ambayo ndiyo mratibu wa Benki zote, njia muafaka iliyoshauriwa ni kuanzisha Benki kupitia SACCOS. Aidha utaratibu wa kuanzisha Benki ya wanawake kwa kupitia kifungu cha matumizi mengineyo ya Wizara kutasababisha Idara isiweze kuendesha shughuli nyengine kutokana na uhaba wa fedha.

**Lengo: Kukuza uelewa wa jamii katika masuala yanayohusu watoto na wanawake**
Katika kukuza uelewa wa jamii juu ya masuala yanayohusu watoto, Idara iliandaa mafunzo ya siku mbili kuanzia tarehe 29/11 hadi 30/11 katika ukumbi wa EA-CROTANAL kwa viongozi wa mabaraza ya watoto ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini. Mafunzo hayo yatawawezesha watoto kuongeza ufanisi katika kuwaelimisha watoto wenzao ndani ya mabaraza kuhusu uendeshaji bora wa mabaraza hayo.

**Changamoto**

Wizara inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa jengo la ofisi, pamoja na rasilimali watu, hivyo huathiri ufanisi wa utekelezaji wa malengo ya Wizara.

**6.8 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA UPANDE WA PEMBA KWA KIPINDI CHA JULAI/SEPTEMBA 2011/2012**

Katika kutekeleza malengo ya Wizara, Afisi kuu Pemba inatumia Seksheni zake tano ambazo ni:-Seksheni ya Mipango, Sera na Utafiti,Seksheni ya Utumishi na Uendeshaji,Seksheni ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto,Seksheni ya Maendeleo ya Vijana na Seksheni ya Ustawi wa Jamii.

**SEKSHENI YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

**UTEKELEZAJI WA MALENGO**.

- **Kuimarisha ukusanyaji wa taarifa, uwekaji wa kumbukumbu na kutayarisha mfumo wa mawasiliano wa Wizara**

Seksheni hii kwa kushirikiana na Idara ya Mipango,Sera na Utafiti Zanzibar imeweza kuandaa mpango wa muda mrefu na muda mfupi wa utekelezaji wa malengo ya Wizara (Bango Kitika) kilichowasilishwa kwa Mhe, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha Seksheni imeweza kutayarisha ripoti na taarifa mbali mbali za mwezi, miezi mitatu, kama vile ripoti ya mpango wa utekelezaji wa kazi na Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2010 – 2015. Ripoti hizi hupelekwa Makao Makuu ya Wizara Unguja, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Ofisi za Wakuu wa Mikoa kwa zile ripoti za Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

- **Kutekeleza Programu ya kupambana na Ukimwi katika maeneo ya kazi.**

Seksheni kupitia Kamati yake ya Jinsia/UKIMWI ya Wizara imeweza kufanya kikao cha siku moja cha Kamati ya UKIMWI, na kuwashirikisha wajumbe wake 11. Katika kikao hicho kamati ilizungumzia utekelezaji na changamoto zinazojitokeza siku hadi siku katika kutekeleza shughuli za UKIMWI/Jinsia katika maeneo ya kazi na shughuli za kila siku kwa Wanawake, Watoto, Vijana, Wazee na Taifa kwa ujumla, ili kunusuru maambukuzi mapya ya virusi vinavyosababisha UKIMWI. Maafisa wameweza kuelimisha wafanyakazi ndani ya seksheni zote za Wizara na makundi ambayo wizara inayafanyia kazi kama vile vikundi vya uzalishaji mali vya wanawake, vijana na wazee.

- **Kukuza uwezo wa Taasisi kuzingatia masuala ya jinsia katika Sera, Sheria, Mipango na Bajeti**

Seksheni ya Mipango Sera na Utafiti imeweza kuzifanyia ukaguzi Kamati za kupinga udhalilishwaji wa kijinsia za Mjini Ole na Tumbe Mashariki, ili kuona namna zinavyofanya kazi zake. Kwa ujumla, Kamati zilionekana kuwa na uwezo mzuri na zinashirikiana na Taasisi mbali mbali katika kupiga vita udhalilishaji wa kijinsia.

Aidha katika suala la kusimamia suala la Jinsia, Kamati ya Ukimwi na jinsia imeweza kutekeleza mkakati wa utekelezaji wa suala la Jinsia katika maeneo ya kazi. Kupitia mratibu wa Jinsia wa Wizara, juhudi za makusudi

zimechukuliwa kuwaandikia kila Wizara/Ofisi za Mikoa na Wilaya kuhakikisha kuwa wanamteua Ofisa Jinsia (Gender Focal Person) kwa lengo la kusimamia suala zima la jinsia kama mkakati wa utekelezaji wa suala hili. Ufuatiliaji na uzinduzi wa kamati hizo tayari umefanyika kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, Wizara ya Katiba na Sheria .Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake imeelezwa kuwa utaratibu huo utaendelea ili kufikia lengo lililokusudiwa.

**SEKSHENI YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

**UTEKELEZAJI WA MALENGO**

- **Kukuza uwezo wa Wizara pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi**

Seksheni imeweza kuwapatia fursa ya kujiongezea ujuzi wa kimasomo wafanyakazi 9 kwa lengo la kufanikisha utendaji wa kazi kwa ufanisi zaidi. Kati ya hao 7 wapo masomoni kisiwani Pemba, mmoja alikuwa nchini Kenya na mfanyakazi mmoja yuko Tanzania Bara. Wafanyakazi hao wako masomoni kwa ngazi tofauti kulinganisha na mafunzo yao, kati ya hao mfanyakazi mmoja anasoma ngazi ya Cheti, 7 wanachukua mafunzo ngazi ya Diploma na wamesaidiwa fedha 1,500,000/- kwa ajili ya ada ya chuo na kila mmoja amelipiwa TSh.375, 000/-

Vifaa mbali mbali vimeweza kununuliwa kwa ajili ya matumizi ya ofisi na kufanyia matengenezo yaliyohitajika vitu kama gari, vespa, pikipiki na kompyuta.

- **Kusimamia masuala ya maslahi ya wafanyakazi wa Wizara**

Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto Pemba ina wafanyakazi 66, kati ya hao Wanawake 33 na Wanaume 33. Seksheni hii imewapatia likizo la kawaida wafanyakazi 10. Wafanyakazi 7 wameweza kupewa malipo ya likizo kati kwa kipindi cha Julai – Sept, 2011. Mfanyakazi mmoja amepewa likizo la uzazi na mfanyakazi 1 yupo likizo bila ya malipo.

Sambamba na hilo Seksheni imeweza kuwatengenezea malipo ya ziada baada ya saa za kazi Wafanyakazi wa Wizara (wakiwemo walinzi, na madereva ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na ikiwa ni sehemu moja ya motisha kwa mfanyakazi).

Aidha Seksheni imeweza kuwatengenezea wafanyakazi Safari za kikazi Unguja na Pemba kwa mujibu wa utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo ya utayarishaji wa mishahara, kuhudhuria vikao vya kamati ya Uongozi na vikao vya Wizara.

**SEKSHENI YA MAENDELEO YA VIJANA**

**UTEKELEZAJI HALISI WA MALENGO**

- **Kukuza Uelewa wa Jamii katika masuala yanayohusu watoto, wanawake, vijana na wazee**

Seksheni imeweza kufuatilia na kutathmini shughuli mbali mbali zilizofanywa na vikundi vya uzalishaji mali vya vijana, ambapo jumla ya vikundi kumi na nne, tisa kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba na vitano kutoka Mkoa wa Kusini Pemba vilitembelewa na kupatiwa ushauri, maelekezo pamoja na mbinu mbali mbali za kuwawezesha kuimarisha, kukuza, na kuendeleza uzalishaji wao, sambamba na kuwataka kuonesha ushirikiano pamoja na kuwa karibu zaidi na Seksheni inayohusiana na maendeleo yao.

Aidha mnamo tarehe 20/07/2011 kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ya Vijana kwa pamoja, Seksheni ilifanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya 2005 ili kuweza kutambua mapungufu yaliomo ndani yake na kuweza kufanya marekebisho kwa ajili ya kuiweka katika hali iliyo bora zaidi, marekebisho ambayo pia yatasaidia katika kuiongezea ufanisi na kasi ya kiutendaji Seksheni ya Maendeleo ya Vijana.

- **Kuendeleza na kuimarisha vikundi vya uzalishaji mali vya vijana kwa kutoa Mafunzo ya ujasiri amali, uongozi na utunzaji wa mahesabu**

Seksheni ya Maendeleo ya Vijana Pemba, imeweza kupata matokeo mazuri ya vikundi vilivyojaza fomu za "UN-HABITAT", ambapo jumla ya vikundi sita kutoka Zanzibar vilichaguliwa ambapo vikundi vinne ni kutoka Pemba na vikundi viwili kutoka Unguja.Mafunzo ya awali yametolewa Unguja kuhusu utumiaji wa fedha watakazopewa vikundi hivyo na wanachosubiri ni kupewa fedha tu ili waweze kuzifanyia kazi. Vikundi hivyo ni (Mshikamano Youth Center, Selemu Women Center, Mkipimiliki na Lion on Development Cooperative Society.)

## SEKSHENI YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO:

### Utekelezaji Halisi wa Malengo

- **Kuimarisha hali za kiuchumi za Wanawake na Vijana kwa kuanzishwa Mfuko wa Vijana na Benki ya Wanawake.**

Seksheni **ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto** kwa kipindi cha Julai –Septemba 2011 imeweza kutembelea vikundi vya Ujasiriamali vya wanawake na kuona maendeleo na matatizo yanayowakabili, pamoja na kuwapatia Mafunzo na ushauri. Seksheni pia imeweza kuvitembelea jumla ya vikundi 48 katika Wilaya zote za Pemba.

Seksheni imebaini kuwa bado vikundi hivyo vinakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo elimu ndogo ya Ujasiriamali na ushirika, kutegemea mradi mmoja ambapo faida yake ni ndogo, baadhi ya vikundi bado havijapata usajili na tayari wako kwenye hatua za usajili, na ukosefu wa mbegu bora za mboga mboga.

Wizara inaendelea na juhudi za kuwapatia mafunzo zaidi wana ushirika wanawake na inashirikiana na taasisi husika katika kukabiliana na changamoto hizo.

- **Kukuza uelewa wa Jamii katika masuala yanayohusu watoto, wanawake, vijana na wazee**

Seksheni imeweza kufuatilia kesi za wanawake zinazoripotiwa kutoka katika familia na zile ambazo ziko Mahakamani na Polisi .Jumla ya kesi/malalamiko 12 zimeripotiwa na kufuatiliwa zikiwemo za kutelekezwa, migogoro ya ndoa, madai, kususiwa, kubakwa na kudhalilishwa.

Aidha hatua mbali mbali kuhusiana na malalamiko hayo zimechukuliwa ili kulinda heshima, utu na haki za wanawake na watoto. Baadhi ya malalamiko ambayo yameripotiwa yamepatiwa ufumbuzi na yale ambayo yanahitaji ufumbuzi wa kisheria wahusika wameshauriwa kuyafikisha katika vyombo vya sheria.

Jumla ya Tshs 323,000/= pamoja na chakula na nguo ziliwasilishwa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watoto Afisi ya Pemba kwa ajili ya huduma za watoto ambao walitelekezwa na baba zao. Vitu hivyo vinawasilishwa baada ya makubaliano baina ya Wizara na wazee wa watoto na tayari wameshapewa wenyewe wazazi.

Aidha Seksheni imeweza kuunda Baraza la watoto katika shehia ya Kinyasini Wilaya ya Micheweni, na kutoa mafunzo elekezi kwa kamati ya uongozi wa baraza hilo. Lengo la kuunda mabaraza hayo ni kuwawekea watoto chombo ambacho watakitumia kwa kutoa mawazo yao katika kusimamia haki zao ndani ya Shehia na pia kutetea haki zao zisivunjwe.

Kwa kipindi hichi Seksheni pia imeweza kuandaa na kutoa mafunzo ya wakufunzi (TOT), kwa wajumbe wa kamati za Jinsia (GBV) wa wilaya, shehia na taasisi mbali mbali. Jumla ya wajumbe 25 wameshiriki katika mafunzo hayo kwa ajili ya kujifunza masuala ya Jinsia, aina za udhalilishwaji, sheria mbalimbali zinazokabiliana na udhalilishaji wa kijinsia na namna ya kuripoti matukio ya udhalilishaji wa kijinsia katika vyombo vya Sheria. Lengo kuu ni kuwawezesha washiriki waweze kutoa mafunzo kwa kamati zao na jamii kwa ujumla baada ya mafunzo hayo ili kesi za udhalilishaji wa kijinsia ziweze kupungua.

## SEKSHENI YA USTAWI WA JAMII

### Utekelezaji halisi wa malengo:-

- **Kuunganisha huduma na miitikio ya wadau katika mambo yahusuyo Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.**

Katika kipindi cha utekelezaji cha Julai/Septemba 2011 Seksheni imeweza kulipa shilingi 840,000/= kwa ajili ya posho la Wazee 8, wanaoishi kwenye nyumba za matunzo Gombani Chake Chake na Limbani Wete. Kwa bahati njema kuanzia mwezi wa Agosti, 2011 wazee wa nyumba za wazee wameongezewa posho kutoka shilingi 25,000/= hadi 40,000/=.

Seksheni hii pia imeweza kuwalipa jumla ya Shs. 4,650,000/- kwa ajili ya posho la waathirika wa Ukoma 62 walioko Makundeni wakiwemo wanaume 32 na wanawake 30, posho hilo wanalipwa kila mwezi. Aidha imeweza kulipa jumla ya Shs.2, 340,000/= posho la watoto na wazee 39 kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Ili kuona kuwa watoto wanapata haki zao za msingi, Seksheni imewalipa jumla Shs. 120,000/= wazee wawili waliojifungua watoto pacha tatu ili waweze kumudu kupata maziwa ya kuwanyonyesha na kukuwa vizuri.

Kwa juhudi za makusudi Seksheni imeweza kuwapatia jumla ya Tshs. 2,550,000/= wazee wa nyumba za wazee wa Limbani na Gombami huduma ya chakula na nguo kwa ajili ya huduma ya Sikukuu ya Id-el fitri. Aidha, Seksheni imetumia jumla ya Tshs. 785,000/= kwa kufanya matengenezo madogo madogo ya majengo katika nyumba za wazee.

Katika kipindi hichi pia Seksheni ya Ustawi wa Jamii imeweza kupokea na kufuatilia malalamiko ya madai ya matunzo ya watoto kutoka katika ndoa zilizotengana, jumla ya madai thalathini na tatu yameripotiwa na tayari kesi thalathini na mbili zimeshapatiwa ufumbuzi na kesi moja inaendelea na majadiliano.

Aidha, Seksheni imepokea jumla ya malalamiko kumi kuhusu matendo ya ubakaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia.

- **Kuendelea kusajili, kufanya tathmini za malipo ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini.**

Katika kutekeleza lengo hili**,** Seksheni imeweza kusajili kesi za Fidia na kupokea malalamiko ya madai ya Fidia kutoka katika wizara za SMZ. Jumla ya kesi tatu zimesajiliwa katika kipindi cha Julai –Septemba. Wizara imeweza kufanya tathmini ya malipo ya fidia kwa kesi zilizorejea hospitali na kupelekwa katika Idara ya Ustawi Unguja, na zimekisiwa kuwa na madai ya Tshs. 6,036,490/95. Sambamba na hilo, wizara imeweza kuwalipa wafanyakazi wawili wanaodai fidia jumla ya shilingi 3,000,000/=.

**Changamoto**

- Uingizwaji mdogo wa fedha.
- Uhaba wa vipando kama vespa na pikipiki kwa ajili ya ufuatiliaji kwa maafisa wa Mikoa na Wilaya.

## 6.9 MAONI YA KAMATI

- Kamati inaipongeza Wizara kuweza kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa ufanisi katika vipindi (kota) viwili vya mwanzo vya utekelezaji wa Bajeti ya 2011/2012 licha ya kuwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti.
- Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha miradi maalum ambayo itasaidia kutoa huduma muhimu kwa jamii hasa watoto na wanawake katika vyuo vya mafunzo ( magereza )
- Wizara kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ishauri kuendelea kupitiwa sheria zote za makosa ya jinai na madai, ili kuondokana na hali iliopo sasa ya kuwekwa mahabusu watoto, wanawake , pamoja na vijana wengi kwa tuhuma za makosa ambayo suluhu yake ingeweza kupatikana katika jamii husika.
- Kuna haja kwa Wizara kuimarisha ushirikiano na chuo cha mafunzo kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki za watoto, wanawake na jamii kwa ujumla zinalindwa kwa kuzingatia misingi ya haki za binaadamu.
- Kamati imebaini kuwa, miongoni mwa mambo yanayochangia kuwepo kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ni kukosekana kwa huduma muhimu za kijamii ikiwemo huduma za afya.Kamati itahakikisha inashirikina na Wizara ya Afya ili huduma za afya ziweze kufikishwa katika maeneo yaliyoathirika kama eneo la KINUNI.
- Kamati imebaini kuwa bado hakuna muamko wa kutosha wa uanzishwaji wa vikundi vya uzalishaji kiuchumi katika maeneo yenye watoto wenye mazingira magumu zaidi.Kamati inatoa rai kwa wizara kushirikiana na wizara ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kuelimisha kina mama ili waweze kuunda vikundi vya uzalishaji, ili viweze kuwasaidia katika kukabiliana na hali ngumu ya maisha katika maeneo yao.
- Kuna umuhimu kwa wizara kuwa na mashirikiano na wizara ya biashara na viwanda kuanzisha maonesho ya kimataifa ya wajasiriamali hasa ya vikundi vya uzalishaji wa bidhaa mbali mbali kwa lengo la kusaidia vikundi hivyo kuwapatia soko na hata kuweza kujitangaza.
- Kamati inaipongeza wizara kwa ubunifu wa kuanzisha Mpango maalumu wa mikopo kwa vijana kwa kushirikiana na benki ya **CRDB**.Hatua hii imesaidia katika kuvijengea uwezo wa kiuchumi vikundi mbali mbali vya kiuchumi nchini. Vikundi hivyo vimeweza kuunda SACOSS moja ya **Zanzibar Vijana Sacoss** itakayotoa mikopo kwa wafanyabiashara na wazalishaji wadogo.Taasisi kama hii tayari imeundwa kwa upande wa Pemba.
- Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kuanzisha ujenzi wa jengo la kudumu la afisi za Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto Pemba ili kuepuka kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kuendelea kutumia majengo ya kukodi.

## 7.0 MAAGIZO

- Wizara isimamie katika kuvihimiza vikundi vya ushirika hasa vile ambavyo vimo katika mchakato wa kufikia masharti ya kufaidika na msaada wa wahisani kama vile msaada wa mfuko wa UN-HABITAT Pemba, kuwa na maeneo rasmi ya kufanyia kazi zao ili kuweza kutambulika kiurahisi na washirika wa maendeleo.
- Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la kukosa ofisi maalumu za kuendeshea shughuli za vikundi vingi vya ushirika Pemba, vikiwemo vikundi vya (Youth Center –Mbuzini na Selemu Women-Wete).Hivyo Kamati inaiagiza Wizara kuvishajihisha vikundi hivyo kuanzisha ofisi rasmi za kazi zao ili kuleta ufanisi zaidi.

- Wizara ichukue juhudi za ziada kuwashajihisha wananchi ambao wameathiriwa na matatizo ya udhalilishaji wa watoto wao kijinsia, kuvitumia vituo vya Mkono kwa mkono (one stop center) ili kuweza kupata huduma za ushauri.

### 7.1 HITIMISHO

Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ni wizara ambayo imekuwa ikijitahidi katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi, licha ya kukabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ndogo. Ni wizara ambayo kiasi cha asilimia 80 ya malengo yake hutekelezeka kupitia michango ya washirika wa maendeleo. Iwapo Serikali imelenga Ustawi wa Jamii kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vyake, kuna haja ya kuipitia ipasavyo bajeti iliyopo ya wizara ili iweze kuongeza ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.